# Nipashe

Jumatano Machi 24, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580529

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





JUMATANO MACHI 24, 2021

Nipashe

ALIVYOENDESHA SIASA NA UONGOZI

**Kadumu na Ujamaa wa Nyerere, katika nyayo alizotumia Sokoine**

## **Anna** Mwakasege; rubani aliyerusha ndege iliyobeba mwili wa JMP Dar- Dodoma



UKURASA 3

## **UN** yaagiza bendera nusu mlingoti siku ya maziko ya Magufuli

UKURASA 3

UKURASA 11

# Bilioni 3.9 washuhudia mazishi kitaifa ya JPM

UKURASA 2




Sehemu ya maelfu ya wananchi wa Zanzibar, waliojitokeza jana, kuupokea mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ambaye aliagwa katika Uwanja wa Amaan. **Picha ndogo:** Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi akitoa heshima za mwisho, huku mmoja wa waombolezaji akiangua kilio. **PICHA: IKULU**






Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

# Dk. Mwinyi: Tumempoteza mwanamapinduzi wa karne

UKURASA 2

**MICHEZO** **NTIBAZONKIZA FITI KUIBEBA YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Bilioni 3.9 washuhudia mazishi ya JPM

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema watu bilioni 3.9 duniani walifuatilia mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Tukio hilo lilifanyika juzi katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma, likiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kuhudhuriwa na marais mbalimbali kutoka nchi za Afrika.

Majaliwa alisema hayo jana mjini Zanzibar wakati wa kuuaga mwili wa wa Dk. Magufuli kwenye Uwanja wa Amani.

"Nashukuru vyombo vya habari mmekuwa nasi toka siku ya kwanza kuonyesha tukio hili na tunazo taarifa kwamba mpaka jana (juzi) jioni, watu waliofuatilia tukio la kuaga mwili jijini Dodoma ni bilioni 3.9 na naamini bado wanaendelea kufuatilia," alisema Majaliwa.

"Nafurahi kuona Watanzania namna mnavyoonyesha mapenzi yenu kwa kiongozi wenu, aliongeza huku akisisitiza kuwa bado nchi iko kwenye majonzi makubwa tangu kilipotangazwa kifo cha kiongozi huyo.

"Nataka niwaeleze Watanzania wenzangu kwamba bado tuko kwenye huzuni kubwa. Tukio hili si la kawaida la kuondokewa na kiongozi aliyekuwa madarakani.

"Tunajua hii yote ni mipango ya Mwenyezi Mungu. Huzuni hii tunayoipata leo ni kwa sababu tulikuwa na imani kwamba tutaendelea naye katika kipindi chote cha uongozi wake kwa mujibu wa Katiba," alisema.

Akizungumzia ratiba ya leo, Majaliwa alisema baada ya mwili kuagwa Mwanza mjini utabebwa kwa gari kwenda kupitishwa katika daraja la Busisi ambalo lilibuniwa na Hayati Dk. Magufuli.

Pia Majaliwa alisema mwili huo utakwenda kusimamishwa kwa muda katika mji wa Busisi ambako ni nyumbani kwa wazazi wa mke wa Hayati Dk. Magufuli.

"Baada ya mwili kuagwa kutoka Mwanza mjini, utapitishwa katika daraja la Busisi alilolibuni yeye mwenyewe Dk. Magufuli na kupitishwa pia kwenye mji wa Busisi ambako ni nyumbani kwa wazazi wa mke wake. Hapo utasimama kwa dakika 10 ili wazee maarufu, ndugu wa mke walioko pale wapate fursa ya kuaga," alisema Majaliwa.

Alisema baada ya kutoka katika mji wa Busisi utapitishwa Sengerema, Katoro, Bwanga, Geita hadi Chato.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Dk. Khalid Salim Mohamed, alisema wananchi wa Zanzibar walifarijika kupata fursa ya kuaga ndiyo maana walijitokeza kwa wingi.

Dk. Khalid alitaja miongoni mwa walioshiriki kwenye tukio hilo la kuaga kuwa ni pamoja mabalozi, viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa, wakuu wa mikoa, mawaziri, wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wabunge, wawakilishi kutoka vyama mashirika ya kimataifa na viongozi wa dini.

Tofauti na ilivyokuwa Dodoma kwa wananchi kuaga kwa kupunga mkono uwanjani na mitaani, wananchi wa Zanzibar walipata bahati ya kila mmoja kupita na kutoa heshima za mwisho.

Kama ilivyokuwa katika maeneo yote ambako mwili huo ulipitishwa kuanzia Dar es Salaam na Dodoma, jana pia Wazanzibari waliulaki mwili kwa wingi, huku wakiimba nyimbo, kutandika nguo na matawi ya miti barabarani.

Licha ya kunyesha mvua, wananchi hao waliendelea kubaki barabarani kutoa heshima za mwisho kwa kupunga mikono huku vilio vikitawala.

Wakati mwili unawasili katika viwanja vya Amani baada ya kuzungushwa katika mitaa mbalimbali, ulilakiwa na kikundi cha watu maalum waliosimama upande wa kushoto na kulia pembezoni mwa msafara uliokuwa ukiongoza mwili, wakiwa wamevalia nguo nyeusi huku wakimwaga maua mpaka pale ulipoteremshwa na kuwekwa katika eneo maalum lililokuwa limeandaliwa kwa ajili ya shughuli ya kutoa heshima za mwisho.



Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, akizungumza na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati wa kuupokea mwili wa Hayati Dk. John Magufuli, kwenye Uwanja wa Abeid Amani Karume, Zanzibar jana. **PICHA: OWM**

# Mwinyi: Tumepoteza mwanamapinduzi

**Na Rahma Suleiman**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewaongoza wananchi wa Zanzibar kuaga mwili wa Hayati Rais John Magufuli, akimwelezea kuwa alikuwa mwanamapinduzi mahiri katika karne hii.

Akizungumza wakati wa maombolezo hayo katika Uwanja wa Amaan Mjini Unguja ambao ulifurika watu jana, Dk. Mwinyi alisema kifo cha Dk. Magufuli kimeacha huzuni na simanzi kubwa katika mioyo ya Watanzania na wapenda maendeleo barani Afrika.

Dk. Mwinyi alisema juhudi kubwa zimefanywa na serikali zote mbili ya Zanzibar na Tanzania ili kuhakikisha Watanzania wanapata fursa ya kuuaga mwili huo na kuonyesha hisia zao na heshima za mwisho kwa mpendwa wao.

"Leo (jana) tupo hapa Zanzibar. Ninataka nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kuja kuaga mwili wa mpendwa wetu," alisema.

Dk. Mwinyi alisema Dk. Magufuli alikuwa mstari wa mbele katika kuimarisha maisha ya Watanzania kwa misingi ya haki na usawa bila ya kujali dini, kabila, rangi wala jinsia. Alisema kifo hicho kimeleta simanzi na wingu kubwa la huzuni kutokana na mapenzi makubwa aliyokuwa nayo kwa Tanzania na Bara la Afrika.

"Kwa hakika, tumepoteza mwanamapinduzi mahiri kwa karne ya sasa. Alikuwa kiongozi mwenye uwezo na kipaji cha aina yake. Kiongozi kama yeye ni nadra sana kupatikana kwa sababu alikuwa kiongozi aliyejipambanua na uzalendo wa kweli, mtetezi wa wanyonge, mwenye kujivunia na kuuonea ufahari utanzania na uafrika wake.

"Dk. Magufuli alikuwa na maono makubwa ya kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua kubwa zaidi za maendeleo kwa kutumia rasilimali tulizobarikiwa na Mwenyezi Mungu.

Dk. Mwinyi alisema Dk. Magufuli atakumbukwa kutokana na hulka njema aliyokuwa nayo ambayo ilitawaliwa na ucheshi, ucha Mungu, bashasha, huruma na mapenzi makubwa kwa Watanzania wote na hukakikisha Tanzania inaendelea kuwa salama na yenye utulivu.

Alisema atakumbukwa kutokana na uongozi wake mahiri uliotukuka hasa kupigania haki za wanyonge, vita dhidi ya rushwa, ufisadi na uzembe.

"Ametuaga akiwa ameiacha nchi katika amani na utulivu wa kupigiwa mfano barani Afrika na duniani kote. Kwa hakika, katika maisha yake, yapo mambo mengi ya kujifunza ya kinadharia na kivitendo yatakayokumbukwa na viongozi, wanafalsafa, wanasiasa, wachumi, wanasayansi na wataalamu wa kada mbalimbali duniani kote," alisema.

Aliongeza kuwa Dk. Magufuli ni zawadi waliyopewa Watanzania na Mungu, akiahidi kuwa Zanzibar itampa ushirikiano Rais Samia Suluhu Hassan katika kufanikisha majukumu yake ya kuwatumikia Watanzania.

## RC atoa angalizo watoto kuaga mwili Kirumba

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amewataka watoto na wanafunzi kutokwenda Uwanja wa CCM Kirumba kwa ajili ya kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati John Magufuli.

Mongella alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na kamati ya maandalizi ya shughuli, kwa lengo la kuepusha vifo na madhara yanayoweza kutokea kutokana na msongamano unaoweza kusababishwa na watu wengi wenye shauku ya kuuaga mwili.

"Idara zote za ulinzi na usalama zimejipanga kuhakikisha ulinzi na usalama unaimarika, na nitoe ombi kwa wazazi na walezi kuhakikisha watoto wanabaki nyumbani wakitazama kwenye runinga, kwa kuwa matangazo yanarushwa kwenye channel zote za ndani," alisema.

Alisema Rais Magufuli ni kipenzi cha watu wa Mwanza na Kanda ya Ziwa, hivyo wanategemea idadi ya watu kuwa kubwa, na kwamba idara zote zinajipanga pamoja na wanaohusika na sekta ya afya.

Pia alisema Chama cha Msalaba Mwekundu na skauti wahakikishe wanakuja watu wazima ili waweze kusaidia pale tatizo linapotokea.

"Mageti ya kuingilia uwanjani yatafunguliwa kuanzia saa 10 alfajiri na mwili utapokelewa uwanja wa ndege saa 1:00 asubuhi ukitokea Zanzibar na utapelekwa uwanjani hapo moja kwa moja kisha sala, dua na maombezi yatafanyika," alisema Mongella na kuendelea:

"Baadaye viongozi mbalimbali wa kitaifa na mkoa watatoa heshima zao za mwisho kisha mwili kuruhusiwa kupitishwa kwenye barabara mbalimbali za Jiji la Mwanza."

# Waziri akatisha kusoma hotuba kwa machozi

**Na Daniel Limbe**, CHATO

VILIO, simanzi na huzuni vilitawala wilayani Chato mkoani Geita jana, wakati wa ibada maalum ya maombolezo ya kifo cha Rais John Magufuli jana.

Katika ibada hiyo, Waziri wa Nishati na Mbunge wa Chato, Dk. Merdard Kalemani, alishindwa kumaliza hotuba yake ya salamu za rambirambi baada ya kububujikwa machozi.

Alikuwa kwenye ibada ya maombolezo iliyoandaliwa na umoja wa madhehebu ya dini wilayani Chato (Chato Inter faith), viongozi na waumini wa dini mbalimbali walijitokeza kwa wingi kwenye viwanja vya stendi ya zamani.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Chato, Charles Kabeho, aliwataka wananchi kumuenzi Hayati Dk. Magufuli kwa kuimarisha amani, umoja na mshikamano aliokuwa anauhubiri wakati wa uhai wake.

"Ninatambua Watanzania tumetikiswa. Kifo cha Dk. Magufuli ni pigo kubwa sana kwa jamii hasa kwa sisi wana Chato lakini kikubwa, tunapaswa kushikamana na kuwa wamoja.


"Januari tulikuwa naye na alituahidi na Mkuu wa Mkoa wa Geita kuwa Aprili atarejea kwa ajili ya kutembelea baadhi ya miradi ya mkoa wetu iliyokwama. Hatukujua kama ndiyo alikuwa akituaga," alisema Kabeho.

"Katibu wa Umoja wa Madhehebu ya Dini wilayani hapa, Mchungaji Clement Kalisti, alisema umoja huo umelazimika kufanya ibada maalum ya maombolezo ya kifo cha Dk. Magufuli kutokana na kutambua mchango wake kwa nchi, madhehebu ya dini na mtu mmoja mmoja.

Rais Magufuli alifariki Machi 17, mwaka huu, kwenye Hospitali ya Mzena Dar es Salaam wakati akipatiwa matibabu ya ugonjwa wa moyo.

# Atembea kilometa 240 kumzika JPM

**Na Alphonce Kabilondo**, GEITA



MGANGA wa tiba asilia, Bugota Bujukano, mkazi wa Bariadi mkoani Simiyu ametembea kwa miguu kwa siku tatu kutoka Bariadi hadi Geita kuhudhuria mazishi ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Mazishi ya Magufuli (pichani), aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam, yanatarajia kufanyika keshokutwa katika kijiji cha Mlimani, Chato mkoani hapa.

Bujukano alisema jana kuwa ameamua kutembea hadi nyumbani kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Waganga na wa Tiba Asili na Ukunga (UWAWATA) Taifa mkoani humo, ili kuungana na waganga wenzake kwenda kwenye mazishi ya Hayati Dk. Magufuli.

Alisema kuwa baada ya kupata taarifa ya msiba, alipatwa na mshtuko mkubwa na kwamba alipokuwa ikisikia vyombo vya habari vikitangaza kuwa mazishi yatafanyika keshokutwa, alianza safari ili kuhakikisha anahudhuria bila kukosa na waganga wenzake.

Mganga huyo alisema waganga wa tiba asilia na Watanzania wamempoteza jemedari wao mwongoza njia aliyekuwa mtetezi wa wanyonge.

Pia alisema Dk. Magufuli katika uongozi wake, alikuwa mstari wa mbele katika kutetea tiba za asili na kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutetea tiba hizo ili kumuenzi kwa vitendo.

"Nimelazimika kutembea kwa mguu kutoka mkoani Simiyu (umbali wa kilomita 240) kwa muda wa siku tatu ili kuungana na waganga wenzangu kwenda Chato kuhudhuria mazishi ya Dk. Magufuli aliyekuwa mstari wa mbele kutetea tiba asilia zitambulike. Waganga tumempoteza jemedari mpambanaji," alisema.

Mwenyekiti wa UWAWATA, John Mahungu, alisema waganga wa tiba asilia na Watanzania wote wamepata pigo kubwa kwa kumpoteza Dk. Magufuli kutokana na uchapakazi wake na kusimamia rasilimali za nchi katika uongozi wake wa kipindi cha miaka mitano.

Alisema tiba asili awali ilidharaulika lakini baada ya Dk. Magufuli kuingia madarakani, alitaka ithaminiwe na serikali kupitia Wizara ya Afya, Idara ya Waganga wa Tiba Asilia, iliwafungulia chuo cha kutoa mafunzo kwa waganga wa tiba asilia, mafunzo ambayo yamesitishwa baada ya kupata taarifa ya msiba.

Mwenyekiti huyo aliwataka waganga wa fani hiyo kujitokeza kwa wingi kuuaga mwili wa Hayati Dk. Magufuli.


AC3 AKIBA COMMERCIAL BANK PLC benki kwa maendeleo yako



Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

SALAMU ZA PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa Akiba Commercial Bank wanaungana na Watanzania wote kumpongeza
Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan
kwa kula kiapo cha kuwa Rais wa sita
awamu ya Tano kwa Serikali ya
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

Hongera sana.


# Wananchi kumwaga JPM kupitia runinga

**Na Richard Makore**, CHATO

SERIKALI imewataka wananchi wilayani Chato na maeneo ya jirani kubaki nyumbani na kufuatilia kwenye televisheni zao tukio la kumuaga, Hayati Rais Dk. John Magufuli, kutokana na eneo la kuagia kutohimili idadi kubwa ya watu.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alitoa agizo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Chato, kuwa uwanja ulioandaliwa kwa ajili ya kumuagia hayati Magufuli ni mdogo na kwamba watu watakaoruhusiwa kuingia ni wachache.

Alisema shughuli ya mwisho ya kuuaga mwili wa Hayati Dk. Magufuli itafanyika kesho Chato na Ijumaa (Machi 26) itakuwa siku ya maziko pekee.

Alisema kesho watakaoruhusiwa kuingia katika uwanja wa mpira wa Magufuli uliopo Kijiji cha Mlimani, wilayani Chato ni viongozi wa serikali wachache, wa dini, wawakilishi wa makundi mbalimbali pamoja na familia.

Aliongeza kuwa wananchi wengine wanatakiwa kubakia nyumbani na kuangalia kwenye televisheni zao.

Aliwataka wananchi hususani wenye matatizo ya kiafya, watoto na wenye ulemavu, kuchukua tahadhari ikiwamo kubaki nyumbani badala ya kwenda kwenye eneo la tukio.

Pia alisema wananchi watapata fursa ya kuaga mwili wakiwa njiani ukitokea mkoani Mwanza.

Alitaja maeneo ambayo msafara utasimama na wananchi kupata fursa ya kuaga kuwa ni Kasamwa, Geita Mjini, Nyankumbu, Katoro, Buseresere, njia panda ya Bihalamulo hadi Chato na kwamba vijiji vyote vya njiani vitapata fursa ya kuaga.

Gabriel alisema maziko yatafanyika Ijumaa katika kijiji cha Mlimani kwenye makaburi ya familia nyumbani kwa Hayati Magufuli na yatahudhuriwa na watu wachache.


Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Joseph Nyamhanga, akizungumza na waandishi wa habari, alisema ujenzi wa eneo la kumuagia Hayati Magufuli umefikia hatua nzuri.

Alisema uwekaji wa mahema na ujenzi wa kibanda maalumu cha kuwekwa mwili wa Hayati Magufuli unakaribia mwisho.

Nyamhanga alisema kazi nyingine zinazoendelea ni uwekaji wa taa, viti pamoja na kufanya usafi.

## MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA)




















# BURIANI

## Dkt. John Pombe Joseph Magufuli

## 1959-2021

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kwa majonzi makubwa, wanaungana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na watanzania wote kuomboleza kifo cha Rais wa awamu ya Tano, Mhe.Dkt John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi 2021.**

**Daima tutauenzi uchapakazi wake, uzalendo, ujasiri, uadilifu, uwazi na uwajibikaji uliotukuka katika kuendeleza sekta ya Bandari Tanzania.**

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. AMINA**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msiba wa JPM uwe somo kwa viongozi

**TANGU** kutangazwa kwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Machi 17, wananchi hususan wanyonge wamemlilia sana, huku wakitoa kauli mbalimbali nzito.

Sote tumeshuhudia jinsi ambavyo umati umekuwa ukijitokeza kwenye shughuli za kuaga mwili huo, kuanzia jijini Dar es Salaam kwa siku mbili Jumamosi na Jumapili. Jumatatu (Dodoma) na jana Zanzibar, kabla ya leo jijini Mwanza na kesho (Chato) na kufuatiwa na Ijumaa ambayo itakuwa siku ya kumpumzisha rasmi Hayati Dk. Magufuli kwenye nyumba yake ya milele kijijini kwake Chato.

Kila Mtanzania amejionea kwa macho yake ama kusikia jinsi umati hususan wa wananchi wanyonge walivyofurika mitaani kwenye barabara ambazo mwili huo ulikuwa ukipitishwa, huku walilia na kutoa kauli za kuonyesha kwamba wamempoteza kiongozi waliyempenda, kumwamini na kumtumainia kuwatatulia matatizo na kero zao.

Waombolezaji wamemuita Hayati Magufuli kwa majina mengi yakiwamo 'chuma', jeshi, 'jembe', 'tingatinga', 'jasiri', 'mtetezi wa wanyonge', 'mkombozi' na mengine mengi. Wamachinga) na bodaboda yalijitosa kuusindikiza mwili barabarani. Hiki ni kielelezo halisi cha ni jinsi gani aliwatumikia na kuwajali wanyonge.

Jumapili, watu kadhaa walipoteza maisha kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kwa kinachoelezwa ni msongamano, ambao ulisababisha hata utaratibu wa kuaga mwili kusitishwa.Mbali na vilio na majina mbalimbali ambayo waombolezaji wamemwita Hayati Magufuli, pia kwa siku zote za kuaga tumeshuhudia makundi ya wanawake na vijana wakirusha kanga, mashati, tisheti na maua barabarani ambapo mwili ulikuwa unapita.

Kadhalika, katika maeneo kadhaa mitaani na kwingineko wananchi wanaendeleza mjadala kuhusu hali ya nchi hususan masuala ya maendeleo aliyokuwa akiyatekeleza kama yataendelea au ndio mwisho wake.

Wanahoji kama mpango wa elimu bure kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha nne utaendelea, mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, uboreshaji huduma za maji, afya, reli ya kisasa, miundombinu na mradi wa umeme wa Nyerere. Mengine kudhibiti ujambazi, vita ya rushwa, uwajibikaji serikalini, matumizi mazuri ya fedha za umma, kwa kutaja baadhi.

Wakuu na wawakilishi wa nchi kadhaa za Afrika waliohudhuria mazishi ya kitaifa jijini Dodoma juzi, wengi walielezea kifo cha Magufuli kuwa ni pigo kwa taifa, huku wakimwelezea kuwa amelifanyia Taifa mambo makubwa kiuchumi, ingawa wameelezea imani kwa Rais Samia Suluhu kuwa atayaendeleza.


Tunaamini viongozi wetu wa serikali wameyaona yote yaliyotokea baada ya JPM kufariki dunia kabla ya kutekeleza mambo yote ya maendeleo ambayo serikali yake iliyaahidi, hivyo msiba wake utakuwa somo tosha kwao; kwamba wanyonge wanategemea mengi na makubwa kutoka kwao.

Tulimsikia juzi Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akishindwa kuzungumza bungeni wakati wa kuaga mwili, akisema alikuwa akijisikia vibaya kuona mwili huo ukiwa umelala mbele yake, lakini somo kwao ni matukio waliyoyaona wananchi wakimuaga Magufuli mitaani na barabarani.

Tunawashauri viongozi wetu wauchukulie msiba huo kama fundisho kwao katika kukidhi matarajio ya Watanzania, hususan kwa kuendeleza mambo makubwa aliyoyaacha ili isionekane ameacha ombwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tumekuelewa vizuri Mama Samia, kikuu wewe rais wetu, tuko pamoja

**TANZANIA** imepata Rais wa Awamu ya Sita ambaye ni Samia Suluhu Hassan, ni baada ya mtangulizi Dk. John Magufuli, kufariki Machi 17 wiki iliyopita.

Hii ni mara ya kwanza kwa Tanzania kupata Rais mwanamke, ambaye kwamba hatua yake kushika nafasi hiyo, inaondoa dhana iliozoeleka katika jamii kwamba wanawake hawawezi kuongoza.

Katika hotuba yake ya juzi jijini Dodoma, wakati wa kuaga mwili wa Hayati John Magufuli, alitoa kauli thabiti inayotoa somo, kutenganisha urais na mwanamke.

Naomba kunukuu: "Naomba niseme kidogo, kwa wale ambao wana shaka, mwanamke huyu ataweza kuwa rais wa Jamhuri ya Muungana wa Tanzania,

nataka niwaambie kwamba, aliyesimama hapa ni Rais....Nataka nirudie kwamba, aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke."

Ni kauli inayoondoa dhana iliyozoeleka ndani ya jamii, kwamba mwanamke hawezi kuongoza, badala yake kutambua kuwa suala la kuongoza si kubeba mzigo kichwani, bali ni kufuata, katiba, sheria, kanuni, taratibu, busara na miongozo ya uongozi.

Rais Samia kuongoza nchi, ni hatua inayoonyesha kuwa usawa wa jinsia ni msingi muhimu kwenye maendeleo ya nchi yeyote ikiwamo Tanzania, kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wanawake na wanaume.

Kimsingi, usawa wa jinsia ni hali ya wanawake na wanaume kuwa na fursa sawa na upatikanaji wa haki zenye kuleta tija, katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya jamii, kati ya makundi hayo mawili ya kijinsia.

Kuwapo usawa wa jinsia, ni kuhakikisha raia wote wanapewa nafasi ya kukua na kuondolewa vikwazo mbalimbali, ili waweze kuchangia na kutambuliwa kwa usawa katika maendeleo yao ya kijamii, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa.

Hivyo, awe mwanamume au mwanamke, yeyote anaweza kuchaguliwa kuwa kiongozi, bila ya kujali jinsi yake, kwa kuwa kama alivyosema Rais Samia, Watanzania wasiwe na hofu na uongozi wake.

Anabainisha kuwa hakuna kitakachoharibika, kwa kuwa amepikwa, ameiva, hivyo ana uhakika kwamba ataitendea haki nafasi hiyo kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na si vinginevyo.

Kama walivyo wanaume, wanawake wana uwezo wa kuongoza kuanzia mwenyekit wa mtaa, diwani, mbunge, katika nafasi za uongozi wa juu wa vyama vya siasa na hata ngazi za juu kitaifa, jambo la msingi ni kuwapa nafasi.

Rais wa sasa alipewa nafasi ya kuonyesha uwezo wake kwa miaka mitano alipohudumu kama msaidizi wa rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli na kuonyesha kuwa wanawake wanaweza.

Nikirejea katika hotuba yake ya kwanza, baada ya kuapishwa, aliwataka Watanzania kujenga na kudumisha umoja wa kitaifa, kwa kupeana faraja na upendo kipindi hiki cha msiba mkubwa.

Huu ni muda mwafaka wa kujenga na kuimarisha udugu wa Kitanzania, amani, utu, uzalendo na utanzania kwa kuyaangalia ya mbele kwa kujiamini na kwa kuwa na matumaini.

Alisisitiza kuwa ni wakati wa kushikana mikono na kusonga mbele kwa ari na moyo mkuu, kufutana machozi na kushikamana katika mchakato wa ujenzi wa Tanzania mpya aliyoitamani Rais Magufuli.

Rais ameshawahakikishia Watanzania na kuwaondoa hofu kuhusu yeye kushika nafasi hiyo, hivyo ingependeza kama jamii itaachana na jinsi yake kutambua kuwa yeye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Iwapo kila mmoja atatambua hilo na kulizingatia, itakuwa ni rahisi kushikamana katika mchakato wa ujenzi wa Tanzania mpya chini ya uongozi wake, ili atimize kile alichokikusudia, kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Ikumbukwe kuwa, dhana kwamba wanawake hawawezi kuongoza, imepitwa na wakati na ndiyo maana hata rais mwenyewe, aliweka wazi kwamba, aliyesimama ni rais na siyo mwanamke.

# WAZANZIBAR WAMLILIA HAYATI JPM



Mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, ukiwasili katika Uwanja wa Amaan, jijini Zanzibar kwa ajili ya kuagwa. **PICHA: IKULU**




Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi akitoa heshima za mwisho kwa Hayati Dk. John Magufuli. **PICHA: IKULU**



Askari wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama, wakipiga saluti wakati ukipigwa wimbo wa Taifa katika hafla ya kumuaga Hayati Dk. Magufuli. **PICHA: IKULU**



Waziri Mkuu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mazishi, Kassim Majaliwa, akizungumza kabla ya kumkaribisha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi kuzungumza na wananchi katika hafla ya kuuaga mwili wa Hayati Dk. John Magufuli katika Uwanja wa Amaan jana. **PICHA: IKULU**



Mwili wa Hayati Dk. John Pombe Magufuli, ukiwasili kwenye Uwanja wa Amaan kwa ajili ya tukio la kuagwa na wananchi wa Zanzibar. **PICHA: PMO**




Wanafunzi wakiwa na bango lenye ujumbe walipojitokeza jana, kuupokea mwili wa aliyekuwa Hayati Dk. Magufuli. **PICHA: IKULU**

UBA
United Bank for Africa

Rest in Peace
H.E. Dr. John Pombe Magufuli
1959 - 2021

The Board of Directors, Management and staff of UBA Tanzania, join the Government, family and fellow Tanzanians as we mourn the passing of his Excellency President John Pombe Magufuli.

His legacy and fruits of his hard work will always be in our memories.

May he rest in eternal peace. Amen



# Wananchi Malawi wamlilia JPM

**Na Thobias Mwanakatwe,** CHITIPA

KIFO cha Rais John Magufuli kimepokewa kwa masikitiko na wananchi wa Chitipa, Malawi.

Wakizungumza na Nipashe katika mji huo jana, wananchi hao walisema Dk. Magufuli alikuwa kiongozi aliyekuwa na mtazamo wa kujenga uhusiano wa kweli, imara na wa kudumu kati ya nchi hizo mbili.

Meshaki Limbewe, mmoja wa wananchi hao, alisema walimfahamu Dk. Magufuli kwa kuwa alikuwa ni mtu wa kazi na mwenye kupenda sana watu wake hasa pale alipoamua kushughulikia kero na matatizo ya watu wa chini.

"Hata sisi majirani zake wa Malawi alitupenda sana, ndiyo maana aliamua kujenga barabara ya lami kutoka Mpemba, Tanzania hadi mpakani pale boda Isongole ambayo imetusaidia sana sisi kufikia soko zuri la mahindi," alisema.



Alisema uamuzi wa Dk. Magufuli kujenga barabara hiyo ulilenga kuimarisha uhusiano wa kweli kati ya mataifa hayo mawili.

James Phili alisema licha ya kutofanikiwa kukutana ana kwa ana na Dk. Magufuli, alimfahamu kama kiongozi imara na mwenye msimamo usioyumba.

"Binafsi ninasononeka sana, lakini kwa kuwa kifo ni jambo lisiloepukika, tunatakiwa sisi na majirani zetu wa Tanzania tukubaliane nalo.

"Kuna wakati unatamani kama kungekuwa na sehemu wanauza spea za moyo, tungenunua turudishe uhai wake," Phili alisema kwa hisia kali.

Phili alitumia nafasi hiyo kuonyesha wasiwasi wake juu ya umaliziaji wa kazi ya ujenzi wa Daraja la Isongole linalounganisha nchi hizo katika Mto Songwe.

"Mwaka huu, alitufanya tuwe na soko zuri la mahindi baada ya ujenzi wa barabara ya lami kutoka Mpemba hadi Isongole kukamilika. Sasa, sijui itakuwaje sehemu ile ya daraja," alisema.

Aliwaomba vingozi wa Serikali ya Tanzania kuona umuhimu na kumalizia sehemu hiyo ya ujenzi wa daraja ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo muhimu kwa ustawi wa maendeleo na biashara kati Malawi na Tanzania.

Serikali ya Tanzania imetumia Sh. bilioni 107.5 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mpemba-Isongole kuunganisha nchi jirani ya Malawi zikiwamo mita 300 ndani ya nchi ya Malawi ambayo ni kiungo muhimu kwa biashara.

WIZARA YA KILIMO
BODI YA KAHAWA TANZANIA

TANZANIA COFFEE BOARD




MHE. DKT. JOHN JOSEPH MAGUFULI
RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
1959- 2021

TANGAZO




Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited imesikitishwa sana na kifo cha Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli atakumbukwa na jumuiya ya GGML kwa uzalendo wake wa dhati, shauku ya kuchochea maendeleo ya Watanzania na pia maono yake madhubuti na thabiti kwa nchi. AngloGold Ashanti - Geita Gold Mining Limited inaungana na Watanzania na waombolezaji wote duniani katika kipindi hiki kigumu.

# NGO zamwomba Samia kusimamia uwajibikaji

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameombwa kuendeleza dhana ya uwajibikaji jamii ili kufanya shughuli za maendeleo kuendelea kushika kasi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Mashirika yasiyo ya kiserikali mkoani Morogoro (NGO), Bonaventura Mtalimbo, alisema jana kuwa kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kimewagusa sana kutokana na kutetea mapinduzi ya kiuchumi, kiutamaduni na hata kijamii nchini.

Alisema Hayati Rais Magufuli alikuwa mchapakazi aliyeacha alama ya uwajibikaji, huku akiwa na hofu ya Mungu, jambo ambalo liliwafanya Watanzania wengi kuwa na dhamira ya dhati ya kujenga nchi.

Alisema mashirika yasiyo ya kiserikali yalishirikiana kwa karibu sana na Hayati Magufuli na kwamba kifo chake kimewaachia ombwe kubwa la simanzi hasa katika masuala ya kuleta maendeleo ya nchi, huku akikumbusha kuwa katika utawala wake ilianzishwa mipango mbalimbali ya usimamizi wa maendeleo yaliyopo ikiwamo usimamizi wa ufuatiliaji wa rasilimali za umma (PETS) na mfumo wa ufuatiliaji uwajibikaji jamii (SAM) katika sekta zote.

Mtalimbo alisema asasi zisizo za kiserikali zilikuwa na wakati wa kufuatilia rasilimali za nchi zilizofujwa baada ya kuwa tayari zimejengwa.

Hivyo alisema ni wakati sasa Rais Samia kuona haja ya kuendeleza dhana ya uwajibikaji ili kila mmoja abaki akiitekeleza kwa maendeleo ya nchi.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na kutoa elimu kwa jamii DIRA Organization, Erasmo Tullo, aliiomba serikali ya sasa kuzidi kufungua milango ya ushirikiano na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kutoa fursa zaidi na kuyajengea mazingira mazuri katika utendaji wao wa kazi.

Alisema ufunguliwaji wa milango ya ushirikiano na mashirika utasaidia kuongeza kasi ya maendeleo kwa jamii mmojammoja na taifa kwa ujumla.

Aidha, Tullo alisema uongozi wa Hayati Magufuli umejenga nidhamu na kuongeza uwajibikaji kwa mashirika yasiyo ya kiserikali kwa kuwa na ufuatiliwaji wa kina wa mara kwa mara.




Mkuu wa Wilaya ya Chato, mkoani Geita, Charles Kabeho (kulia), akipokea moja ya mabati 180 kutoka kwa Meneja wa NMB, Kanda ya Ziwa, Baraka Ladslaus (katikati), kwa ajili ya Shule ya Sekondari Bongela, wilayani humo mwishoni mwa wiki. Benki hiyo imetoa madawati 110 kwa ajili ya shule za msingi Ihanga na Kakeneno, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 12.6. Kushoto ni Meneja wa NMB Chato, Festo Issanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Club yapunguza mimba za wanafunzi

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

CLUB ya wanafunzi katika Shule ya Sekondari Salawe Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ambayo ina jihusisha na utoaji wa elimu ya makuzi na afya ya uzazi, imesaidia kupunguza tatizo la mimba za wanafunzi shuleni hapo.

Mkuu wa shule hiyo, Faraja Mbilinyi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari ambao wanatekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT).

Mbilinyi alisema mwaka 2019 alipohamishiwa shuleni hapo kikazi, alikumbana na tatizo la wanafunzi 19 kupewa ujauzito na kuacha masomo, lakini baada ya kuanzishwa club ya wanafunzi, mimba za wanafunzi zimepungua na kutokea tatu kwa mwaka tofauti na zamani.

"Hatua ambayo tuliichukua kama shule kukabiliana na tatizo hili la mimba za wanafunzi ni kuanzisha club kwa ajili ya kutoa elimu ya makuzi, afya ya uzazi, na madhara ya kujamiiana katika umri mdogo, hali ambayo imesaidia kupunguza kasi ya mimba shuleni hapa," alisema Mbilinyi.

Mmoja wa wanafunzi, Paulina Fabian, anayesoma kidato cha nne, alisema club hiyo imesaidia wanafunzi wengi kujitambua pamoja na kutoa taarifa pale wanapokuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili na hatimaye wahusika kichukuliwe hatua mapema kabla ya kuleta madhara.

Diwani wa Kata ya Salawe, Joseph Buyugu, alisema katika kutatua tatizo hilo la mimba za wanafunzi, walikaa na viongozi wa serikali na kupitisha mikakati ikiwamo kuwakamata wahusika na kuwawajibisha kupitia jeshi la jadi Sungusungu pamoja na kuwatenga kwenye kijiji, hali ambayo imesaidia kupunguza mimba za wanafunzi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka wanaume kuacha tabia ya kuwarubuni wanafunzi na kujamiiana nao, bali watafute wanawake wenye rika lao ndio washiriki nao tendo hilo na siyo watoto wa shule, huku akionya serikali itaendelea kuwashughulikia ambao watawapa ujauzito wanafunzi.

## Neema yanukia kwa wanawake wachimba madini

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya kuendeleza wachimbaji wadogo wa madini (FADev), inatarajia kuanza utoaji wa fedha za ruzuku kwa wanawake wachimbaji wa dhahabu mkoani Shinyanga.

Pia watapatiwa mkopo wa vifaa vya uchimbaji bila riba, ili kuwakuza kwenye sekta hiyo na kuwainua kiuchumi.

Mratibu wa miradi wa taasisi hiyo, Evance Lubara, alibainisha hayo jana wakati wakitambulisha Mradi wa Jinsia kwenye sekta ya madini, kwa lengo la kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu kwenye uchimbaji wa madini, ambao utatekelezwa mkoani Shinyanga, kwa kuanza na migodi iliyopo Msalala wilayani Kahama.

Alisema katika mradi wao wa jinsia, wamejipanga kuwawezesha wanawake kuwaunga kwenye vikundi vya ujasiriamali ambao ni wachimbaji wadogo kisha kuwapatia fedha ili wapate m i -taji ya kuendesha shughuli za uchimbaji madini, pamoja na vifaa vya uchimbaji bila riba na kuinuka kiuchumi.

"FADev tumeanza kuwezesha wanawake ambao ni wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwapatia fedha za ruzuku kwa ajili ya mitaji, ambapo tuta anza na kuwezesha kutoa Sh. 500,000 hadi milioni moja kupitia kwenye vikundi, na watakao kuwa wakifanya vizuri wataongezewa ruzuku," alisema Lubara.

Katibu Mtendaji wa FADev, Tina Mwasha, alisema katika mradi huo, watawapatia pia wanawake elimu ya ujasiriamali, wakiwamo na wanaume ili fedha wanazozipata waziwekezwe kwenye miradi mingine ya maendeleo na kukua kiuchumi.

Mwasha alisema mbali na kuwezesha wanawake, pia watakuwa wakitoa elimu kwa wachimbaji wote wadogo wa madini, namna ya utunzaji wa mazingira, usalama kwa kuvaa vifaa kinga, kuacha matumizi ya kemikali, pamoja na kutunza taarifa za mauzo ya madini, ili wakopesheke kwenye taasisi za kifedha.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoani Shinyanga, Tedyson Ngwale, alisisitiza kwenye uwezeshaji huo wanawake wachimbaji wadogo wa madini wapewe zaidi vifaa vya uchimbaji madini kuliko fedha, ili kuondoa changamoto ya ulaji fedha hizo za ruzuku.




ALIVYOENDESHA SIASA NA UONGOZI

# Kadumu na Ujamaa wa Nyerere, katika nyayo alizotumia Sokoine

**Na Peter Orwa**



Rais Dk. John Magufuli, alipokagua maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa, mkoani Morogoro. **PICHA: MTANDAO**

KATIKA sehemu ya kwanza, jana iliichambua mfumo na mikakati ya kuendesha elimu ya nchi, iliyoendeshwa na hayati Rais Dk. John Magufuli. Je, mfumo wake alivyoiendesha taifa kisiasa na kiuongozi, ulikuwaje?

Hapo kuna mtazamo mtambuka, ambao unabeba sura mbili. Moja ni kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) alikokuwa pia mwenyekiti, akiongozwa na sera na ilani ya uchaguzi alikojinadi na kumpitisha.

Hapo kisiasa kutoka katika chama chake CCM na hata itikadi binafsi, iko bayana Dk. Magufuli ni muumini mzuri wa muasisi wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere katika mtazamo wa kijamaa.

Hapo kunaweza kukawapo haja ya kuwa sawa, tafsiri au dhana halisi ya Ujamaa, inamaanisha nini, ikizingatiwa ni miongo kadhaa sasa haipo, ikizidi kuchukua sura ya nadharia zaidi katika zama zilizopo.

Kwa mujibu wa tafsiri aliyopenda kuirejea kila mara. Mwalimu Nyerere, alimaanisha kwa matamashi; "Ujamaa ni mfumo wa maisha ya watu kuishi pamoja, kufanya kasi kwa pamoja kwa faida ya yote."

Pia, aliyekuwa mwanazuoni na mchambuzi mahiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam(UDSM), marehemu Profesa Haroub Othman, aliufafanua Ujamaa kwamba unagawayika katika sura kuu tatu, mojawapo ni huo alioufafanua Mwalimu Nyerere.

Mingine anaitaja ni uliotoweka kwingi duniani unaojulikana kama Ukomunisti, ambao ulikuwapo sana katika nchi za Asia kama China, iliyokuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kisovieti (USSR) na baadhi ya sehemu za Ulaya Mashariki.

Hapo kunakuwapo ukiritimba mkuu wa serikali kumiliki rasilimali, lakini kigogo mkuu wa kiuchumi na inaendesha uchumi dola kwa kuibeba wajibu wa kuhudumia watu wake katika mengi, kama vile afya na elimu na hata falsafa za kiitikadi.

Kinyume cha msimamo, ni uhuru wa soko huria na kila mmoja anajihudumia zaidi katika mahitaji yake, Mwalimu Nyerere akiutafsiri kuwa Ubepari.

Pia, Profesa Othman, aliitaja aina ya tatu ya Ujamaa ni pale katika nchi zenye sura ya uchumi huria kama za Magharibi duniani, serikali inakuwa karibu na kuchukua kuhudumia maslahi ya watu wake.

Hiyo mara nyingine huwa zinaitwa mfumo wa uchumi wa mlengo wa kushoto, wakati wa kibepari unaitwa mlengo wa kulia.

Katika Ujamaa huo wa tatu, aliyekuwa mhadhiri wa sayansi ya siasa wa UDSM, raia wa Sudan Kusini, Dk, Alfred Lokuji, anaufafanua kwa matamshi: "Serikali inakuwa sehemu ya umma, kamwe haiwezi kubaki kando watu wake inaingilia kati kuwanusuru kutoka kuelemewa na gharama za soko."

Mfano wake hai, ni pale serikali inapotoa ruzuku au kufuta au kupunguza baadhi ya gharama ya mzigo wa gharama kwa umma, kama vile kwenye matibabu.

Ndani ya utashi huo wa kisiasa, Dk. Mafuguli alikuwa mjamaa aliyefuata nyayo na itikadi za Mwalimu Nyerere kwa kiasi kikubwa hivi sasa akiwa ndani ya staili ya tatu ya Ujamaa, aliyoufafanua Dk. Lokuji, katika 'vigezo na masharti' vya Mwalimu Nyerere, vya uongozi wake.

Pia, katika ulingo halisi wa siasa zake, akiwa katika nafasi yake ya Mwenyekiti wa chama chake CCM, hakujitokeza sana katika nyendo za chama za kila siku.

Mwenyekiti Dk. Magufuli, kwa kiasi kikubwa majukumu makuu ya chama, ikiwamo propaganda za kila siku, aliwaachia Makamu Wenyekiti, Philip Mangula (Bara) na Dk. Ally Mohamed Shein (Visiwani) na timu yake ya Sekretarieti chini ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally.

Hao ndio walioonekana zaidi kumaliza mengi ya kisiasa na yeye alijitokeza zaidi katika mathalani yaliyo rasmi kiutendaji kama vile vikao vya vipindi maalum na vile vya dharura na matukio makuu.

Kwa sehemu kubwa, alijikita katika 'hapa kazi tu' kama Rais. Hata itakumbukwa aliweka bayana pindi tu alipoingia madarakani kwamba, suala la mabadiliko ya katiba hayakuwa kipaumbele katika zama zake za uongozi, mbadala wake akijikita katika kujenga nchi.

## STAILI YA KUWAJIBIKA

Kuna sura kadhaa za ufanyaji kazi, kisiasa akiwa muumini wa Ujamaa na msimamo wa Mwalimu Nyerere, lakini ambaye itikadi zake alizitekeleza katika mazingira ya sasa.

Kuna baadhi ya mambo aliyaendesha bila ya kupinda, bali aliyabeba kama yalivyo. Hapo kuna azma ya kuhamia Dodoma, Ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na vita dhidi ya rushwa.

Pia, katika mfumo wa milki za mali ya umma, mengi ya utekelezaji wake ulikuwa katika sura kutaka kurejesha miliki ya mali ya umma, kupitia namna ilivyokuwa mashirika ya umma kuanzia zama za ufilisi wake, mwaka 1967, kupitia Azimio la Arusha.

Vivyo hivyo, kuna sura ya pili iliyobeba hulka na misimamo yake binafsi, kwamba alikuwa mkali pasipo kutoa nafasi kwa mkosaji aendae kinyume na sera, maagizo yake ya umma na sheria kwa jumla.

Staili yake ya menejimenti kwa kiasi kikubwa, aliitumia kile wasomi wa taaluma hiyo wanaiita Nadharia 'X' ambayo kuna usimamizi wa moja kwa moja, tena huenda

INAENDELEA UK.12



# Kadumu na Ujamaa wa Nyerere, katika nyayo alizotumia Sokoine

INATOKA UK.11

unachukua sura ya 'kijeshi' kufuatilia kuhakikisha kazi husika inakamilika.

Nadharia 'Y' huwa ni usimamizi wa kidiplomasia, mtendaji kwa kiasi kikubwa akijisimamia ndani ya maelekezo aliyopewa. Inashuhudiwa kwa wataaluma kama walimu, madakatari na hata madereva.

Ila katika kuweka utendaji kwenye mstari, Dk, Magufuli, alikuwa mfuatiliaji wa karibu wa maelekezo na uwajibikaji wa utendaji wa watumishi wa umma.

Wapo waliodiriki kumliganisha na satili yake hiyo ya ufuatiliaji na aliyvokuwa, Hayati Edward Sokoine, aliyewahi kuwa Waziri Mkuu na aliifariki mwaka 1984, kipindi kifupi Dk, Magufuli alipokuwa mhitimu wa masomo ya ualimu, chuoni Mkwawa, Iringa.

Katika hilo, kuna wakati Hayati Dk, Magufuli alidiriki kuwa wazi wazi kwa kutoa simulizi namna alivyowapigia simu za kikazi usiku wa manane baadhi ya watendaji wake, ngazi za mawaziri na makatibu wakuu.

Viyo hivyo, akaanika namna alivyofuatilia mawasiliano yasiyo na tija ya kimtandao baina ya watumishi na penye msuguano aliingilia kati na kuwakosoa.

Kupitia matendo ya aina hiyo, Dk. Magufuli hapo anaacha alama nyingine ambayo alikuwa muwazi na hakuficha jambo, kwa lililo na maslahi ya umma.

Kama alivyokuwa hayati Sokoine, Dk. Magufuli, mtindo wake wa kazi Dk. muda wote alifuatilia kwa karibu na kusimamia aliyoyataka, akitumia nadharia ya menejimenti ijulikanayo kama 'X' na wakati huo huo alipenda kuhakikisha ukweli wa jambo hilo.

Aliibuka na nadharia 'Y' pale tu mhusika anamridhisha kwa vitendo kwamba anaendana na kasi yake, jambo ambalo anadaiwa alilionyesha sana katika baraza lake la mawaziri awamu ya pili iliyopo sasa.

Ndio ilikuwa staili ya Hayati Sokoine na hata ikirejewa umauti uliomkuta, Aprili 12 mwaka 1984 mkoani Morogoro, alikuwa akikagua hali ya kilimo nchini katika staili ya kufuatilia uhalisia, akitumia usafiri gari kutoka bungeni Dodoma, kuelekea Dar es Salaam.

Muda wote katika maisha yake kazini, Dk. Magufuli amekuwa mfuatiliaji wa karibu wa kila jambo ama analisikia, anahisi au anataka kujiridhisha. Ni tabia aliyodumu nayo tangu kwenye utumishi akiwa Mkemia Mkuu wa Ushirika Nyanza, alikoanza mwaka 1989.

Aliendelea nayo akiwa waziri, hata kuna wakati aliwafuatilia



Rais Dk. John Magufuli, alipokagua maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa, mkoani Morogoro.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Ushuhuda wa Dk. Magufuli, uko licha ya wasifu wa kutokuwa mtembezi nje ya nchi juzi katika mazishi yake mjini Dodoma, viongozi wa kimataifa, walionyesha kumhusudu namna alivyoishi nao.



Rais Nyerere, alipokuwa na Waziri Mkuu wake, Edward Sokoine.

kwa kujificha watumishi wa kituo kimoja cha mizani ya magari mkoani Pwani, akashuhudia urasimu na matukio ya rushwa, hata akawachukulia hatua.

### ANAVYOAMUA

Akibaki katika nadharia yake ya 'X' katika picha ileile ya ukali wa Sokoine, wote wakirithi kwa namna moja au nyingine kutoka kwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, hakuwa karibu sana na kutoa nafasi kwa nadharia 'Msalie Mtume' dhidi ya mkosaji wa msalahi ya taifa.

Staili yake ya uamuzi, ulikuwa wa papo kwa hapo na ndipo simulizi za 'kutumbua' zilipochukua nafasi yake na hasa katika yanayofanana na rushwa hakuwa na masihara hata kidogo.

Ni zama ambazo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, ilishika kasi ikiashiria vita dhidi ya rushwa ilikuwa juu kama alivyotamka Mwalimu Nyerere, alivyokuwa nayo na hata 'kumkosakosa' mmoja wa waziri wake.

Ni katika tafsiri hiyo hiyo, Sokoine aliendesha vita dhidi ya walanguzi, ambayo ilitikisa nchi, wafanya magendo na wala rushwa wa zama hizo kwa mujibu siasa iliyokuwapo zama hizo, waliangukia pagumu.

Katika utendaji wake, palishuhudiwa wengi katika historia wakifikishwa na wakati huohuo, alikuwa mwepesi wa kutoa misamaha mingi ya kimahakama.

### STAILI YA UTEUZI

Staili yake kiutendaji, daima akiwa kiongozi wa kisiasa hakujiwekea mipaka ya uteuzi wa kugota CCM pekee.

Alishuhudiwa namna alivyoteua wanasiasa waandamizi kutoka kambi ya upinzani kuunda timu ya serikali yake, ambao ni Anna Mghwira, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Profesa Kitila Mkumbo, kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji (sasa (waziri) na David Kafulila aliteuliwa, kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe

Pia, hulka yake nyingine ambayo ni mpya kitaifa, alikuja na staili aina yake ya kupenda kuwateua wasomi wenzake wa ngazi za maprofesa na wenye shahada za uzamivu (Phd) wakitambulishwa kwa vishangilio vya daktari, kama alivyokuwa yeye, aliwapa dhamana mbalimbali kuongoza.

Na hiyo imekuwa kuanzia ngazi za uwaziri hadi taasisi na wakala wa kiserikali, tena wengi katika maeneo yao ya kitaaluma, huku katika maeneo aliyoamini yana mahitaji maalum, aliteua askari.

Hadi sasa kuna maeneo kama Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), iko chini ya mkuu kutoka Jeshi la Ulinzi wa Wananchi, akitumia askari a jeshi hilo kwenye mahitaji.

### URAFIKI KISIASA

Wakati leo ni mafuriko na mikiki mkoani Mwanza kumuaga Hayati Dk. Magufuli, anaacha alama kubwa ya kuwa mzalendo wa kweli na hata akaonyesha urafiki kwa jamii yote.

Ushuhuda wa Dk. Magufuli, uko licha ya wasifu wa kutokuwa mtembezi nje ya nchi juzi katika mazishi yake mjini Dodoma, viongozi wa kimataifa, walionyesha kumhusudu namna alivyoishi nao.

Mfano ni pale Filipe Nyusi, Rais wa Msumbiji alipoejea walivyopigiana simu mapema asubuhi, Dk Magufuli akimtaka awahi kwenda kuchapa kazi, namna ya uhusiano ambao Rais Nyerere alikuwa nao na Rais Samora Macel; wa nchi hiyo. Ni aina ya ushuhuda ambao nao, swahiba wake kutoka Kenya, Rais Uhuru Kenyatta.

Nchini, kuna somo la aina yake kwamba alikuwa Mkatoliki, aliyekuwa rafiki na kipenzi cha kweli wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), makao makuu na mkoani Dodoma, wote wakitoa ushuhuda wa ukaribu na kusadiana, ikiwa ishara kuu ya utendaji wa siasa uliojaa uzalendo dhahiri.

Kwa ujumla ni kifo kinabeba mengi ya darasa la kisiasa, katika uzalendo, uwajibikaji na upendo wa kweli.

***Fuatilia ulingo mwingine unaomhusu kesho, katika sekta tofauti.***





# MWANZA WAZIZIMA NA MSIBA

- RC: Tukubali, tuungane kuomboleza
- Mwanazuoni: Sina shaka na Rais Samia
- Viongozi wa dini: Tumepoteza, tukubali

**Na Neema Emmaunel,** MWANZA

"HAKIKA chema hakidumu." Ni kauli iliyotolewa na viongozi wa dini na wafanyabiashara wakati wakimlilia hayati Dk.John Magufuli.

Ni kifo kilichogusa makundi mbalimbali ya Mwanza. Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti Mwenza Kamati ya Amani Mkoa wa Mwanza, Sheikhe Hassan Kabeke, anasema Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mkoa wa Mwanza wamepokea kwa masikitiko taarifa ya msiba wa kiongozi huyo wa kitaifa.

Anasema, aliyofanya ni karama aliyokuwa amepewa na Mungu kama zawadi na alitumika kama zawadi kwa Watanzania, kwa staili ya unyenyekevu na kwa moyo mpaka alivyokutwa na mauti bila ya kuwa na hiyana.

Hivyo, anawataka Watanzania kuwa watulivu katika kipindi kigumu cha sasa, sanjari na kuyaenzi mema aliyoyafanya katika uhai wake, kwani historia ya nchi haijawahi kutokea kiongozi wa juu kufariki akiwa madarakani.

"Mwenyezi Mungu amesema kila nafsi itaonja mauti pia natoa pole kwa Mufti Mkuu wa Tanzania Sheikhe Abubakar Zuberi Ali," anasema Kabeke.

Pia, anatumia fursa hiyo kuwaomba vijana wanaotumia mitandao ya kijamii 'kuposti' yaliyo ya amani wakimwombea aendelee kubaki katika mioyo ya Watanzania.

Askofu wa Kanisa la C.E.C(T) Charles Sekelwa, anasema Rais Magufuli, alikuwa anaishi katika maneno aliyoyasema na ameacha alama na kielelezo, kwa kusimamia jambo na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika.

Anasema amewarithisha mambo mema watu wake, kwa maana ya kuongoza, uchapakazi, kushinda tamaa ya mali, mtetezi wa haki kwa wanyonge na hakubagua tajiri wala maskini.

Hivyo aliwaomba Watanzania kutokukata tamaa, washikamane na wajihadhari kwani wakati wa shida inapotokea kwenye Taifa kama Tanzania, ambayo imeishi kwa amani kwa kipindi chote, maadui wa nje walio wengi wanaweza kupenyeza mambo yao.

Askofu anasisitiza ni kipindi cha maombolezo, hivyo viongozi wa dini wa kiimani wahamasishe waumini wao katika nyumba za ibada kushikamana na Taifa litabaki salama.

Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa Mwanza, Askofu Philipo Mafuja wa wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) Dayosisi ya Mwanza, anasema Mungu ameamua kumpumzisha Rais Dk. Magufuli na kutupatia Rais Samia Suluhu tuendelee kuyaenzi yale yote yalioachwa na Hayati Magufuli.

Imamu Mkuu wa Msikiti wa Ijumaa mkoani Mwanza, Sheikh Hamza Mansoor, anasema Allah, ameamua kutoa mtihani kwa tukio hilo la kuondokewa na Rais, hivyo anakumbukwa kwa kuyaenzi aliyoyafanya na kuthamini mchango wake.

Rai yake ni kuuombewa Rais Samia Suluhu Hassan. Afanikishe hoja ya kuongoza nchi.

#### WAFANYABIASHARA

Wakizungumza na Nipashe, wafanyabiashara wa soko kuu jijini hapa, Mwajuma Hussein na Baraka Kizimili, wanasema watamkumbuka hayati John Magufuli kwa mengi, likiwamo vitambulisho vya mjasiriamali, kwani alionyesha kuwajali na kuwathamini watu wa chini kwa kila la maendeleo .

"Hadi sasa siamini kweli Magufuli ametuacha ukweli usiku wa jana, watu wengi hatukulala, nilipopata taarifa nilishituka presha ikapanda ikabidi nilambe glukosi, hakika ametuacha wakati tunamuhitaji sana, ona hiyo miradi aliyoiacha ukweli tutamkumbuka alifanya kazi kweli "anasema Hussein.

Said Tembo, ni Mwenyekiti wa Shirika la Umoja wa Machinga jijini Mwanza, anasema kifo hicho, ni pigo kubwa kwao, kwani alikuwa mtetezi wao, aliwalinda, aliwafanya wajiamini na aliwahakikishia hawatopata shida.



Sheikh wa Mkoa wa Mwanza, Hasani Kabeke, akitoa ufafanuzi kuhusu kifo cha Rais, Dk. John Magufuli. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

#### VIONGOZI MKOA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, wakati wa kikao cha maandazi ya kumuaga Hayati John Magufuli kilichowahusisha Kamati ya Amani na Ulinzi ya Mkoa, anasema

Mkoa wa Mwanza kupitia viongozi wa dini umekuwa na utulivu mkubwa, baada ya Rais Samia Hassan Suluhu kutangaza kifo cha Dk. Magufuli.

"Tumeondokewa na mpendwa wetu baada ya kuungua kwa muda mfupi kwa tatizo ambalo tumegundua ameugua kwa muda mrefu. Serikali ya Mkoa inatambua mchango wa viongozi wa dini tuendelee kuwa wamoja na kuiombea nchi yetu," anasema Mongella

Pia, anafafanua kuwa wakati uliopo ni mgumu anaomba viongozi wa dini mkoani Mwanza, kuhamasisha wananchi utulivu katika kipindi cha maombolezo ya msiba sanjari na kujitokeza kwa wingi kumuaga Hayati Magufuli leo.

#### WADAU MKOA

Naye Meneja Shughuli na Usafirishaji wa Ushirika wa Nyanza, John Masalu, anasema daima watamkumbuka kwa mengi, ikiwamo kurejesha mali zilizoporwa na kuchangia Nyanza kulegea, lakini baada ya kuzirejesha sasa Nyanza wako imara.

"Tutamkumbuka sana kama mfanyakazi mwenzetu tulifanya naye kazi vyema pia kwa upande wangu niliajiriwa naye mwaka mmoja hakika tumepoteza shujaa," anasema Masalu.

Mchambuzi wa Siasa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Dotto Bulendum, anasema ni wakati Watanzania wanapaswa kuondoa hofu na mtazamo kuhusu usimamizi na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo na masuala mbalimbali ya nchi.

Anasema Watanzania hawapaswi kuwa na hofu kuhusu utekelezaji wa maono ya Hayati Rais Dk. Magufuli, anaamini Rais Samia Suluhu Hassan, atatekeleza majukumu hayo kwa weledi mkubwa akiongozwa na katiba na ilani ya chama chake.

Anasema Rais Samia, tangu alipoingia kwenye siasa mwaka 2000 alionyesha uwezo mkubwa wa utendaji kwenye masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, hivyo hapaswi kutiliwa shaka.

Pia Rais Samia anachotakiwa, ni kusimamia Katiba na ukimtizama tangu ameingia kwenye siasa mwaka 2000, amekuwa akipanda na nyota yake kung'ara kila siku, hivyo ni kiongozi mwenye uthubutu asiyetiliwa shaka, atafanya vizuri akisaidiwa na watu wanaomzunguka.

Anaongeza kuwa kiongozi huyo na Rais wa nchi mwanamke wa kwanza katika historia ya Tanzania, amewahi kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba kipindi ambacho kulikuwa na joto kubwa la mchakato wa mabadiliko ya katiba, alionyesha uwezo wa hali juu na anaingia kwenye nchi iliyo na mifumo thabiti licha ya msiba imetulia.

"Akiamua kutumia katiba hiyo hakuna kitakachomkwaza kwa sababu tayari Hayati Rais Magufuli, alishafanya mabadiliko ya kimfumo na sera, alifanya mabadiliko ya sera na sheria ya madini, sheria ya kodi ambayo ilikuwa ni tatizo kwa nchi yetu na usimamizi wa rasilimali za nchi.

"Hivyo akisimama kwenye mifumo hiyo,watakachokikosa Watanzania ni haiba ya Rais Magufuli, lakini maono yake yatafikiwa na nchi itakwenda,"alisisitiza Bulendu.

Mhadhiri huyo wa SAUT, anasema Rais Samia atazifikia na kuzitimiza ndoto na maono ya Hayati Rais Dk. Magufuli za kuwafikisha Watanzania kwenye uchumi wa juu kwa kutekeleza sera ya viwanda jambo ambalo alitamani kuona linaleta manufaa kwa wananchi kuzalisha kupitia viwanda na kujiajiri.

### SHAIRI KUMUENZI JPM

## TUNYAMAZE TUSILIE

Kwa nguvuzakeManani, Kalamuninaishika
Nikiwanaohuzuni, msibaulotufika,
Hatunayeduniani, Mja wake katutoka.
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

Funzokwawatanzania, kwelitumewaidhika
Kwa yaliyotufikia, kwamatashi ya Rabuka
Hakunawakubakia, mautiyatatufika
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakossa

Narudiahiimada, vizurikueleweka
Uhaijambo la muda, zamuyakoikifika
Tudumukwenyeibada, tupatezakebaraka
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

Ni ya kwakemaamuzi, katuhanamshirika
TumetokakwaMwenyezi, Muumbaalotukuka
Na walahanaajizi, rohoyakoakitaka
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

Twajuasimuonezi, Munguametakasika
Hayupomwenyeujuzi, kuhojialolitaka
Hachelewimaamuzi, wakatiukishafika
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa


HakikakwakeKarima, wajandikotumetoka
Na kurejealazima, hilohalinamashaka
Tumuombemwishomwema, tupatekunusurika
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakossa

Tayaenziyalomema,yalealiyoyataka
Wizi, rushwa, nahujuma, mnoalikasirika,
Adhabubilahuruma, alitoakwaharaka
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

Uchumiuloimara, alitakakujengeka
Viwandavyenyeubora, kwabidhaahitajika
Tuviuzekilakona, nchiipateinuka
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

Alotwaausukani, mpekherinafanaka
Mwepushiemitihani, umkingenafaraka
Aidumishe Amani, umojakuimarika
Tunyamazetusilie, Molahafanyimakosa

**Na:**
**Jamal Adam (Mpirira)**
**Bodi ya Kahawa Tanzania**
**Moshi**





JUKWAA LA UONGOZI

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

# Mrithi wa JPM anayegota safu ya juu 'kinamama tunaweza' kwa vitendo

• Tamko moja, lajibu minong'ono mamia

**Na Christina Mwakangale**

JUZI hotuba yake ya pili tangu kuapishwa, akiwa katika tukio la kumuaga Rais Dk. John Magufuii, aliyefariki wiki iliyopita jijini Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan, ilikuwa ya kipekee katika wadhifa huo

Wakati kwanza, alihutubia katika mazingira mara tu baada ya kuapa kuwa rais, jana ilikuwa na mazingira yaliyozama zaidi.

Kwanza, 'alifunguka' mengi ya moyoni katika namna ya alivyomfahamu marehemu Dk. Magufuli, mbele ya wageni wake, marais na wawakilishi wa viongozi wa nyadhifa hizo kutoka nchi 10 marafiki wa Kiafrika

Lakini, lililowakosha wengi, kinamama zaidi na hata kinababa, ni pale alipovunja ukimya kuhusu mustakabali wa kijinsia na hata minong'ono mbele ya umma, kitaifa na kimataifa, kuhusiana na dhana 'itakuwaje Rais mwanamama.'

Alisafisha hisia zote kwa tamko la kijasiri, kwamba: "Naomba niseme kidogo kwa wale ambao walikuwa na shaka na mwanamke, huyu ataweza kuwa Rais wa Tanzania. Nataka niseme, aliyesimama hapa ni Rais!"

Baada ya kutamka hilo, alikaa kimya kwa muda fupio, huku umma uliofurika katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma, ukilipuka kushangilia, tena wake kwa waume, aliendelea: "Nirudie kusema, aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!"

Kimsingi, Rais Samia, anaweka historia baada ya kuwa mwanamke wa kwanza kuiongoza nchi katika nafasi ya Rais na Makamu wake, upatikane uhuru mwaka 1961, hata upande wa pili wa Muungano.

Mama Samia (61), aliapishwa na Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma Ijumaa wiki iliyopita Ikulu jijini Dar es Salaam, tukio lililoendana sana na itifaki ya kupigiwa mizinga 21 na akakagua gwaride maalumu kwa mara ya kwanza, akiwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Barani Afrika na kimataifa kwa jumla, kulishuhudiwa mengi ya uongozi wa kinamama, ikianza na mwanamke wa kwanza barani humo, kuwa Rais Ellen Johnson Sirleaf wa Liberia na aliiongoza Liberia kwa miaka 12, licha ya kwamba kuna wakati utawala wake ulibezwa kwa kashfa mbalimbali.

Duniani, kuna rekodi inaonyesha Rais wa kwanza mwanamama duniani, ni Vigdís Finnbogadóttir, wa Iceland aliyeingia madarakani mwaka 1980 na alikaa kwa miaka 16.

Barani Afrika kuna nchi zaidi ya 50 za Afrika, ni wanawake watano tu waliowahi kushika wadhifa wa urais, wakiwamo Sylvie Kiningi (Burundi), Ellen Joyce Banda (Malawi), Ameenah Gurib Fakim (Mauritius)na Sahle-Work Zewde (Ethiopia).



Samia Suluhu Hassan, alipoapa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

> Ninadhani kikubwa kinachotakiwa ni kujenga mifumo imara wa kuwapata wale wataoweza kuvaa viatu vya wale watakaomaliza muda wao kisheria na kwa mujibu wa Katiba.

Ni mfano tosha wa namna kinamama wanavyoleta matokeo chanya na makubwa katika nchi zao, kupitia uongozi wao. Hapo kuna mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi nchini, kuanzia miaka ya 1990 kunakojumuisha mkutano wa dunia kuhusu wanawake, huko Beijing, China.

Ni mkutano ulioleta mageuzi ya mapinduzi ya kijinsia na ndipo wanawake wakaanza kuonekana kwenye taasisi mbalimbali, pamoja na ongezeko la wabunge wanawake bungeni.

Rais Samia alianza kung'ara kwa upekee, pale alipoteuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba la mwaka 2014, lililofanyika mjini Dodoma.

Mama huyo anaingia katika urais, wakati ni mwezi ulioadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, yaani Machi 8 ya kila mwaka.

Siku ya Wanawake huadhimishwa kukumbuka tukio la tarehe 28 Februari, mwaka 1909, New York nchini Marekani, wanawake walikoandamana kutaka malipo ya mshahara sawa na wanaume, kutokana uhalisia kwamba wanafanya kazi sawa na wanaume.

Hapo ndipo likazaa wazo la kuadhimisha rasmi kila tarehe hiyo, kukachukuliwa kama tarehe ya kimataifa ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Ikiwa sehemu ya jamii nayo, Tanzania iliadhimisha kwamba, matukio mbalimbali yakiongozwa na wanawake.

Kaulimbiu ya mwaka huu ilikuwa ni 'Wanawake katika Uongozi Chachu ya Kufikia Dunia yenye Usawa.'

Alipohudhuria maadhimisho hayo jijini Dar es Salaam, akiwa mgeni rasmi, bado katika wadhifa wa Makamu wa Rais, aliukumbusha umma kutoa fursa kwa wanawake kutoa maamuzi.

Mama anasema kwamba, pengine kungekuwapo mafunzo namna ya wanawake kushika nafasi za uongozi, basi yangeanza mafunzo ya kuondokana na kasumba zenye madai mwanamke hawezi kuongoza.

Rais Samia anashauri pia yatolewe mafunzo kwa wanawake, kuhusu jinsi ya kupata na kushika nafasi mbalimbali , ili kuongeza ushiriki wao katika kufanya uamuzi.

Anasema kwamba, ili kuhakikisha wanawake wanaongezeka kwenye nafasi za uongozi, kwa kuwa bado kuna tatizo, akiwataka wanawake kila wanapozungumza mambo yao na kupanga kutatua changamoto na kuondoa vikwazo, waache kulalamika bali wayatatue.

Rais Samia anasema duniani kote, mwanamke kwa kiwango cha juu wamezungukwa na madhila tofauti na kuwakwamisha maendeleo yao.

Kuhusu maendeleo, anasema fursa ziooa kiuchumi, kisiasa anataja uko usawa na kwamba Tanzania ijikite katika kumuondolea mwanamke vikwazo.

Anamtaja mwanamke ni nguzo inayopaswa kujengwa kwa madhubuti, ili kupata maendeleo na nguzo yake pekee ni kuwa na mazingira wezeshi kwa wanawake kwa jumla.

Katika takwimu anazozitaja kwenye maadhimisho hayo, anasema wanawake wana uwezio wa kuwa chachu ya maendeleo na hiyo inatokana na uhalisia wanawake wako asilimia 51 wananchi wote, huku wanaume wako asilimia 49.

"Wanawake nchini iwe chachu na mwanzo wa mageuzi katika maendeleo kupata uongozi kuifikia dunia yenye usawa," anasema.

**NGUZO YA MAMA**

Mikataba inayoongoza na kuelekeza hatua mbalimbali za kufuatwa ili kupinga na kuondoa ukandamizaji dhidi ya wanawake na hatimaye kuleta usawa katika nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mchambuzi wa kisiasa, Abbas Mwalimu, ambaye pia ni mtaalamu wa diplomasia, anasema Desemba, 1979 Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, lilipitisha Azimio Namba 34/180 lililozalisha Mkataba wa Kimataifa unaopinga aina zote za ukandamizaji dhidi ya wanawake kwa kifupi CEDAW, iliyoanza kufanya kazi rasmi tarehe 3 Septemba, mwaka 1981.

Anasema, ni mkataba unaozitaka nchi wanachama kuweka kanuni ya usawa baina ya wanawake na wanaume katika katiba za nchi zote wanachama, sambamba na kuweka mazingira bora yanayohakikisha kanuni hiyo inatekelezwa.

Lingine ni kuwekwa na kuchukuliwa mazingira mahsusi tya kikatiba, ikiwa ni pamoja na kuweka vikwazo dhidi ya wanaowakandamiza wanawake kwa kuzuia aina yoyote ya ukandamizaji dhidi yao, wanawake.

Anasema mkataba wa CEDAW unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua maalumu zisizo za kudumu au za muda mfupi, zinazolenga kuleta usawa wa kiuhalisia baina ya wanawake na wanaume.

"Nina imani kubwa wanawake wanaweza sana kuleta mabadiliko chanya katika vyombo vya uamuzi wakiwezeshwa na kujiwezesha.

"Ninadhani kikubwa kinachotakiwa ni kujenga mifumo imara wa kuwapata wale wataoweza kuvaa viatu vya wale watakaomaliza muda wao kisheria na kwa mujibu wa Katiba," anasema Mwalimu.



## Wanawake, vijana wapewa mbinu fursa za kilimo

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

TAASISI inayoshirikina na wadau kuboresha mifumo ya masoko (AMDT) imetoa mafunzo kwa wakulima wanawake na vijana kutambua fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo, kulima kwa tija na kuongeza thamani ya mazao ili kushindana na soko.

Ofisa Mtendaji wa taasisi hiyo, Charles Ogutu, alibainisha hayo jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye semina na majadiliano juu ya fursa zilizopo kwenye sekta ya kilimo.

Ogutu alisema kuwa sekta ya kilimo nchini inajumuisha theluthi mbili ya Watanzania, lakini mchango wake katika pato la taifa bado kidogo sana.

Alisema wanawake na vijana kama watawezesha elimu kutambua fursa zilizopo kwenye kilimo wataweza kulima kwa tija na kushindana na soko la mazao ya kilimo.

"Tunataka kuwafundisha wanawake pamoja na vijana kwa kuwa wao ndiyo kundi kubwa katika taifa letu kama watafanikiwa kutambua fursa zilizopo kwenye sekta hii ya kilimo basi taifa litapiga hatua wanawake siku zote ukiwafundisha kitu wanafanya vizuri sana kuliko wanaume," alisema Ogutu.

Pia alisema wanawake na vijana hawatakiwi kuendelea kushiriki katika kilimo kimazoea bali wabadilike katika mitazamo yao ambapo wataweza kulima kwa tija na kujikwamua kiuchumi," alisema.

Aidha, alisema ili kufikia Tanzania ya viwanda, kilimo kinatakiwa kupatiwa kipaumbele na kundi kubwa litakalofanikisha hali hiyo ni vijana na wanawake.

"Vijana ndiyo wenye nguvu na ndiyo idadi kubwa katika taifa hata teknolojia hizi za kisasa wao wanaweza kuzitumia ipasavyo hivyo kwa kuwapatia elimu ya kutambua fursa zilizopo kutafanikisha kufikia malengo yao," alisema.

Vile vile, alisema kuwa umefika wakati sasa pia mazao ya kilimo kama mahindi na mengineyo yauzwe kwa njia za kisasa kama vile masoko mtandao (Digital Market).

Theodora Pius, kutoka mtandao wa vikundi vya wakulima wadogo (MVIWATA), alisema kuwa matatizo makubwa ya wakulima nchini ni pamoja na upatikanaji wa masoko ya mazao yao na ardhi.

Mjumbe wa Bodi ya Chama cha Wanawake Wafanyabiashara (TWCC), Victoria Mwanokuzi, alisema wanawake wengi wamekuwa wakishindwa kutokana na kukosa elimu kuhusu mambo mbalimbali.

Alisema katika semina hiyo wamewafundisha wanawake mbinu mbalimbali za kufanikisha shughuli zao za kilimo pamoja na uanzishaji wa viwanda vya usindikaji wa bidhaa zitonakazo za kilimo.

"Wanawake wengi walikuwa wanalalamika kuhusu mitaji lakini tumewaeleza sisi kama chama cha wafanyabiashra wanawake nchini tumeingia mkataba na Benki ya NMB na CRDB hivyo wanaweza kupata mikopo yenye riba ya asilimia 14," alisema.

Meneja wa Tawi la CRDB, UDOM, Ditrick Mdoe, alisema wao kama taasisi ya fedha wamekuwa wakitoa mikopo kwa ajili ya wakulima na wasindikaji wa mazao ya kilimo kama alizeti.

"Katika hili changamoto tunazokutana nazo ni wakulima kushindwa kufanya mambo yao ndani ya muda, hivyo wakati mwingine kuchukua mikopo wakiwa wamepishana na msimu wa mazao, hivyo leo tumewaelimisha muda gani sahihi kwao," alisema Mdoe.

# Watu wenye ulemavu wamkumbuka JPM

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WATU wenye ulemavu wamesema watamkumbuka Hayati Rais Dk. John Magufuli kutokana na mambo makubwa ya maendeleo aliyoyafanya nchini, ikiwamo kutoa mikopo ya asilimia mbili kutoka katika halmashauri.

Wakizungumza na Nipashe baada ya kuaga mwili wa Hayati Rais Dk. John Magufuli walisema kifo chake kimewagusa sana, hivyo wataendelea kumuenzi kwa mambo mbalimbali ambayo alikuwa akiyasisitiza watu wafanye ili kupata maendeleo.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake Abdul Yusuph, alisema kuwa Hayati Magufuli aliwafanyia mambo makubwa ikiwamo kuwapa mwakilishi serikalini ambaye anapigania na kuwasemea matatizo yao ili yapatiwe ufumbuzi.

Yusuph ambaye ni mlemavu wa viungo, alisema moja ya mambo ambayo yalifanywa na Hayati Rais Magufuli ambayo hawatayasahau ni ile asilimia mbili ya mikopo ya wenye ulemavu ambayo hutolewa na halmashauri mbalimbali.

Yusuph, alisema fedha zile za mikopo zimeleta matunda makubwa sana kwenye kundi la walemavu kwa sababu imewasaidia kuendesha shughuli zao za biashara ambazo zimewasaidia kujiinua kiuchumi.

"Sisi watu wenye ulemavu hatumsahau jinsi alivyotuthamini tunaamini Rais Mama Samia Suluhu, atafuata nyayo zake," alisema Yusuph.

Alisema ni jambo ambalo kwao ni vigumu kusahaulika kutokana na kile kilichofanywa na serikali wakati wa uhai wake.

Mbali na hilo, alisema kitendo cha Hayati Magufuli kuwapatia mwakilishi katika Baraza la Mawaziri kimerahisha kero zao kutatuliwa pale wanapoziwasilisha.

Alisema kutokana na hali hiyo wanamwombea kwa Mungu apate pumziko la milele huku wakiwaombea aliowaacha waweze kutimiza azma aliyoikusudia enzi za uhai wake.

Naye mama mjasiriamali Husna Hassan, alisema kwa upande wa kinamama watamkumbuka kwa mengi kwa sababu amekuwa mstari wa mbele kuwasikiliza kero zao hususani akiwa katika ziara zake za mara kwa mara katika mikoa mbalimbali. Husna alisema kujaa kwao Uwanja wa Jamhuri ni moja ya sababu ya kumkumbuka kwa mazuri aliyokuwa akifanya kwa wananchi wake.

"Tutaendelea kumkumbuka kila iitwapo leo, ametusaidia sana ikiwamo kutuhimiza kufanya biashara kwa ajili ya kujiinua kiuchumi," alisema Husna.

Kwa upande wa kijana Julius Mlela, alisema vijana wana kila sababu ya kuhudhuria kuaga mwili wa hayati mpendwa Rais Dk. John Magufuli kutokana na kile alichowafanyia wakati wa uhai wake.

Alisema jambo hilo linazidi kuwatia huzuni mioyoni, ambapo alisema wanaamini waliobaki hawatayaacha makundi hayo kwenye harakati za maendeleo.




Aliyekuwa Mgombea Urais kupitia Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa, akisaini kitabu cha maombolezo cha kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, eneo la Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## ...Wazee wamkumbuka kwa huduma za afya

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

KATIBU wa Shirika la kusaidia Wazee Tanzania (SAWATA) Mkoa wa Dodoma, Oswin Kachenje, amesema watamkumbuka Rais John Magufuli, kutokana na kuwaboreshea huduma za afya wazee nchini.

Alisema hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu kifo cha Rais huyo kilichotokea Machi 17, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Kachenje, alisema wazee nchini watamkumbuka Rais Magufuli kutokana na kuboresha huduma kwa kundi hilo ambalo lilikuwa na malalamiko ya miaka mingi.

"Sisi wazee kama kuna kitu hatutamsahau Rais Magufuli, ni kilio chetu cha miaka mingi kudai huduma bora za kiafya kwa wazee kwenye maeneo ya hospitali na vituo vya afya," alisema.

Alisema wakati wa utawala wake huduma hizo zimeboreshwa kwa wazee kutengewa dirisha maalum pamoja na kupewa kipaumbele kila wanapofika kwenye maeneo mbalimbali ya kutolea huduma.

"Siku hizi ukifika sehemu za kutolea huduma utakuta kuna tangazo limeandikwa mpishe mzee kwanza apate huduma hiyo ni heshima kubwa aliyotupa Rais wetu Magufuli," alisema.

Pia alibainisha kuwa matangazo kama hayo yalikuwapo siku za nyuma, lakini hayakutiliwa mkazo kama kipindi hiki cha utawala wake.

Aidha, alisema wazee hao wa Mkoa wa Dodoma wanaungana na Watanzania wengine katika kuomboleza msiba huo kwa sababu umeligusa taifa.

Kadhalika, alisema kuna misiba ya viongozi wengine ilitokea lakini huu wa Rais Magufuli ni wa kipekee kwa sababu kifo chake kimetokea akiwa madarakani.

Aliongeza kuwa kutokana na hali hiyo imelifanya taifa kushikwa na hofu kubwa kwa sababu kimetokea ghafla na kila mtu anajiuliza utaratibu ukoje wa kuwapata viongozi wengine.

Alisema sababu kuu ya hofu ni kutokana na mazoea ya viongozi wote waliopita kupatikana na kwa njia ya kupigiwa kura kwenye uchaguzi mkuu ambapo kila mtu aliwapima kutokana na sera za vyama vyao.

Hata hivyo, alisema SAWATA inaungana na Watanzania wote katika kuliombea Taifa kuwapata viongozi waadilifu watakao saidiana na Makamu wa Rais baada ya kuapishwa kushika nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.





# Wasema watamkumbuka daima JPM

**Na Nebart Msokwa, ILEJE**

BAADHI ya wananchi wa Malawi, wamesema watamkumbuka aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, kwa kuwajengea daraja linalounganisha nchi yao na Tanzania katika Mpaka wa Isongole wilayani Ileje.

Wananchi hao walisema jana kuwa kiongozi huyo amelifanyia maendeleo makubwa taifa la Tanzania katika kipindi kifupi na kwamba baadhi ya maendeleo hayo yamewanufaisha, ikiwamo barabara ya Mpemba-Isongole.

Mmoja wa wananchi hao, Meshack Mkondya, alisema kifo cha Dk. Magufuli kiliwashtua kutokana na kwamba hawakuwahi kusikia kwamba alikuwa anaumwa.

Alisema kiongozi huyo amejenga daraja linalounganisha nchi hizo mbili ambalo linawasaidia kusafiri bila shida kutoka nchini mwao kwenda katika miji ya Tunduma, Isongole na Mpemba kununua bidhaa mbalimbali.

"Hili daraja litatufanya tumkumbuke sana huyu kiongozi. Tumekuwa tukisafirisha mazao yetu kuja kuuza kwenye soko la Isongole kwa kupitia kwenye hili daraja, lakini hata barabara hii inatusaidia sana," alisema Mkondya.

Naye James Pili ambaye alikuwa anazungumza zaidi lugha ya Kichewa, alisema Magufuli alikuwa mchapakazi ambaye anastahili kuigwa na viongozi wengine wa mataifa ya Afrika. Alisema ndani ya muda mfupi wa uongozi wake, ameibadilisha Tanzania.

Alisema kuna miundombinu ambayo imejengwa Tanzania kwa muda mrefu ilikuwa inaonekana kwenye mataifa machache ya Afrika hasa Afrika ya Kusini na Misri.

Pili alisema katika kipindi chake kulikuwa na uhusiano mzuri kati ya Tanzania na Malawi, hivyo akamuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuendeleza uhusiano huo kwa kuwa wananchi wa nchi hizo wamekuwa na mwingiliano mzuri hasa maeneo ya mpakani.

"Sisi wananchi wa Wilaya za Chitipa na wa Ileje kwa muda mrefu tumekuwa na uhusiano mzuri na kila mwaka tumekuwa tukifanya sherehe za ujirani mwema. Sasa tunamwomba Rais mpya wa Tanzania aendeleze uhusiano huu," alisema Pili.

Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Joseph Mkude, alisema wananchi wengi wa Malawi wamekuwa wakifurahia uhusiano wa mataifa haya mawili hasa wakati Dk. Magufuli akiwa hai kutokana na mazungumzo yaliyokuwa yanaendelea.

Alisema Dk. Magufuli alifanikisha ujenzi wa barabara ya Mpemba-Isongole yenye urefu wa kilomita 51.3 ambayo inaunganisha nchi hizo mbili, hivyo barabara hiyo ina faida kwa mataifa yote mawili.

"Hata daraja la Mto Songwe lililojengwa na serikali ya Tanzania linawasaidia na linawashangaza maana hawakutarajia kwamba lingejengwa ndani ya nchi yao, walidhani pengine tungeisubiri serikali yao," alisema Mkude.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Songwe, Mhandisi Yohane Kasaini, alisema barabara hiyo ya Mpemba-Isongole imekamilika isipokuwa ujenzi wa daraja la Mto Songwe bado unaendelea.

Alisema daraja hilo likikamilika litasaidia kuongeza ushirikiano wa kibiashara kati ya mataifa hayo mawili hasa kupitia mpaka huo wa Isongole.



Wachuuzi wa ndizi wa Mji wa Kiwira, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya, wakiwa na bidhaa zao, wakisubiri wateja jana, ambao asilimia kubwa ni abiria wa magari yanayofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Kyela.. PICHA: NEBART MSOKWA

# Matrekta yadaiwa kusababisha ajali

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

MATREKTA madogo, maarufu kwa jina la Power Tiller, yanadaiwa kusababisha ajali nyingi wilayani Mbarali kutokana na kuendeshwa nyakati za usiku bila kuwa na taa.

Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Mbarali, January Mahundi, alisema juzi kuwa baadhi ya madereva wanatumia tochi za simu za mkononi kuona wakati wakiendesha matrekta hayo kwenye barabara kuu, hivyo kuhatarisha maisha yao na ya watumiaji wengine wa barabara.

Alisema kuna matukio ya ajali ambayo yamesharipotiwa polisi ya matrekta hayo kugongwa na magari mengine au kuwagonga watumiaji wengine wa barabara nyakati za usiku kutokana na kutokuwa na taa.

"Power tiller nyingi hazina taa. Madereva wanaoyaendesha nyakati za usiku baadhi yao wanalazimika kutumia tochi za simu za mkononi ili kuona wanakokwenda, jambo ambalo limeshatusababisha ajali nyingi," alisema Mahundi.

Mahundi alisema kuwa changamoto kubwa ya matrekta hayo yasiyo na taa ipo hasa maeneo ya vijijini ambako vijana wanaendesha matrekta hayo bila kuzingatia sheria za usalama barabarani hasa nyakati za usiku na hivyo kusababisha ajali.

Aliwataka viongozi wa vijiji hasa wenyeviti wa vitongoji kuchukua hatua kwenye maeneo yao kwa kutoa elimu ya usalama barabarani ili kunusuru maisha ya vijana wao na watumiaji wengine wa barabara.

"Wenyeviti wa vitongoji ni vizuri tukawa tunatoa elimu kwa watumiaji wa vyombo vya moto. Sisi kama wasimamizi wa sheria tunakutana na changamoto nyingi kwa hawa wanaotumia hivi vyombo vya moto.

"Mfano hivi karibuni wakati tunafanya operesheni usiku tukakutana na mtu anaendesha power tiller akiwa amelewa chakari, huku chombo chake cha moto kikiwa hakina taa na badala yake yeye mwenyewe amewasha tochi ya simu yake na kuifunga kichwani ili aweze kuona mbele, hili ni jambo la hatari sana," alisema Mahundi.

Mwenyekiti wa Mamlaka Mji Mdogo wa Rujewa, Chameta Godigodi, alisema waanza kufanya msako na kutoa elimu kwa wananchi ili kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani jwa kushirikiana na mamlaka husika.

Aliwahimiza madereva wa vyombo hivyo vinakuwa na taa na vifaa vingine ambavyo vinalinda usalama wa dereva na abiria.

## Wahitimu mafunzo ya dawa za usingizi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANAFUNZI 36 wa mafunzo ya utoaji wa dawa za usingizi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), wamehitimu mafunzo ya mwaka mmoja na kutunikiwa vyeti.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, aliwatunukiwa vyeti vya kuhitimu mafunzo na kuishukuru serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa kutoa idhini ya kuanzishwa kwa shule hiyo mwaka 2019.

Alisema mafunzo hayo yamesaidia kukabiliana na uhaba wa wataalamu wa dawa za usingizi kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma na kuwasihi wanaporudi kwenye maeneo yao ya kazi, kuendeleza ujuzi, elimu na ushirikiano ili kuboresha huduma za upasuaji nchini.

"Raha ya kufanya kazi katika chumba cha upasuaji ni kila mmoja kuona umuhimu wa mwenzake bila kujali ngazi ya elimu yake. Mnaporudi mkafanye kazi kwa ushirikiano na kutambua umuhimu wenu na wa mengine na kujikita katika mbinu nyingine ya kujiongezea kipato ili kustawisha uchumi binafsi," alisema Dk. Mbwaji.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wenzake, Sabina Mwilongo kutoka Kituo cha Afya cha St. Vincet Vikindu, Mkuranga mkoani Pwani, aliushukuru uongozi wa hospitali hiyo kuanzisha mafunzo ya utoaji dawa za usingizi ambayo yameongeza maarifa ya namna ya kuwahudumia wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji.

Mkuu wa Idara ya Ganzi na Dawa za Usingizi wa MZRH, Dk. Amos Muzuka, alisema kuwa wahitimu hao zaidi ya kupatiwa mafunzo ya utoaji salama wa dawa za usingizi, walipatiwa ujuzi katika idara mbalimbali ikiwamo ya wagonjwa walio katika uangalizi maalum (ICU) na idara ya magonjwa ya dharura na ajali.



## Wataalamu tiba asili watakiwa kujisajili

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Mufti wa Zanzibar imewataka wataalamu wa tiba asili wanaotumia dawa za Kisuna na aya za Quran kujisajili katika ofisi hiyo ili kufanya kazi zao kwa misingi inayokubalika bila kuvunja utamaduni na silka za Zanzibar.

Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema wakati alipokuwa akizungumza na wadau wa tiba asilia ofisini kwake Mazizini kwa lengo la kuwatambua na kufahamu sehemu wanaofanyia kazi zao.

Alisema ofisi yake ina haki ya kusimamia shughuli zote zinazofanywa katika kusomea watu dua, ruqya pamoja na kutoa dawa za kisuna kwa kuwa imebainika zinafanywa bila kufuata utaratibu.

"Nataka utaratibu ufuatwe mjisajili ili muweze kufanya kazi zenu kwa ufanisi katika kufanya visomo," alisema.

Pia alisema ofisi ya Mufti inapaswa kujua idadi ya waganga wanaotoa dawa za Kisuna Zanzibar, shughuli zao na kuwashauri kufuata utaratibu na nidhamu wakati wa kufanya kazi zao.

Alivitaka vyombo vya habari kutowaruhusu waganga wa dawa za Kisuna kutoa matangazo kwenye radio zao mpaka wawe wamesajiliwa rasmi vinginevyo vinaweza kufungiwa.Naye Mkurugenzi Utawala, Mipango na Rasilimali Watu, Othman Mohamed Saleh, alisema suala la kusoma dua limekuwa na mtihani mkubwa hivi sasa na kwamba bila ya usajili hakutakuwa na ufanisi mzuri.Alisema makosa mengi wanayaona na kama wahusika wa kusimamia masuala hayo hawawezi kunyamaza kwa kuwa wakikaa kimya watakwenda kuulizwa na Mungu.Wakitoa michango yao, waganga wa dawa za kisuna, walisema wako tayari kufuata utaratibu pamoja na nidhamu zilizowekwa na ofisi ya Mufti na kuacha kuoneana wivu ili kujenga ushirikiano wa kuwasaidia wananchi na kumuogopa Mungu.

# Wananchi Mjini Magharibi kuendelea kumuenzi JPM

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrissa Kitwana Mustafa, ameongoza wananchi, viongozi wa serikali na vyama vya siasa wa mkoa huo kutia saini kitabu cha maombolezo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Akizungumza baada ya kutia saini, Mustafa alisema wananchi wa Zanzibar hususani wa Mkoa wa Mjini Magharibi wataendelea kumuenzi kiongozi huyo na Jemedari wa Tanzania kwa kuziendeleza kwa vitendo falsafa zake ikiwamo ya kuchapa kazi kwa kufanya kazi kwa bidii na kuleta maendeleo.

Alisema Watanzania wamejawa na huzuni kwa kuondokewa na kiongozi wao waliyempenda na mtetezi wa wanyonge na kutoa wito kuendelea kumuombea dua apumzike salama katika makazi yake ya milele.

"Kwa kweli ni msiba mzito umemgusa kila Mtanzania, lakini na Afrika kiujumla, hakika kazi ya Mungu haina makosa, tunachopaswa kila mmoja amuombee Mungu kwa imani yake apumzike salama huko aendako, hakika kuondoka kwake kuwe fundisho kwetu," alisema.

Baadhi ya viongozi na wananchi wametoa wito kwa Watanzania kuendelea kushikamana katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo ya mpendwa wao ili taifa lisonge mbele.

Wamewaomba Watanzania wote kumwombea dua na kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa kufanyakazi ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo zaidi.

Naye Mwinjilisti wa Kanisa Katoliki (KKKT) Mwanakwerekwe Zanzibar, Benjamin Sudayi, alimwelezea hayati Dk. Magufuli kuwa muda wote alimtanguliza Mungu katika kuwatumikia Watanzania na kuacha fundisho na alama kubwa kwa wananchi aliowaongoza kwa kumwamini Mungu kila hatua ya maisha yao.



Mmoja wa wananchi wa Zanzibar waliokuwa wamejipanga barabarani kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Karume hadi Uwanja wa Amaan, akipungia mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, jana. PICHA: IKULU

# ...Wana-CCM wamkumbuka kwa mageuzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WENYEVITI wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar wametoa salamu za rambirambi kwa makamu wenyeviti wa chama hicho Bara na Zanzibar kufuatia kifo cha aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho taifa, Dk. Magufuli wakikumbuka mageuzi makubwa yaliyofanywa katika kipindi chake na matokeo yake chama kuimarika kiuchumi na kujitegemea. Wakizungumza kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi Unguja kichama Mohamed Rajab, alisema aliyekuwa mwenyekjiti wa chama hicho taifa alionyesha matumaini makubwa kwa CCM na kufufua uhai wa chama kushika hatamu na kuongoza dola.

Rajab alisema katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa Dk. Magufuli katika nafasi ya wenyekiti wa chama, alikuja na mabadiliko makubwa ambayo yalileta ufanisi na kukiwezesha chama kujitegemea na kuacha kutegemea ruzuku.

"Tumejifunza mambo mengi katika kipindi cha uongozi wa Mwenyekiti Dk. Magufuli, ambaye alikuja na mabadiliko makubwa ya kukiwezesha Chama Cha Mapinduzi kujitegemea kimapato na kiuchumi hatua ambayo ilirudisha matumaini kwa watendaji wake," alisema.Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Haji Ame, alisema chama kimepata pigo kubwa kwa kuondokewa na mwenyekiti wake mwenye uwezo, ubunifu na mikakati ya kukiendesha chama kisayansi zaidi.Alisema CCM kwa upande wa Zanzibar kiliimarika katika kipindi cha miaka mitano na kukiwezesha kuwa imara hatua ambayo imekifanya kushinda uchaguzi mkuu wa Oktoba kwa kishindo na kura nyingi."Katika kipindi cha uhai wa Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi CCM umeimarika zaidi hatua ambayo imekifanya kushinda katika uchaguzi mkuu na kushika hatamu ya kuongoza dola," alisema.Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Unguja, Ramadhan Abdalla, alisema huu ni wakati wa kujenga mshikamano zaidi ndani ya chama hicho kufuatia kuondokewa kwa mwenyekiti wake.Alisema katika kipindi chake cha miaka mitano Dk. Magufuli alijenga mshikamano mkubwa ndani ya chama hicho ambao matokeo yake, chama kuimarika kiuchumi pamoja na mapato, kusimamia na kutekeleza ilani yake hadi ushindi katika uchaguzi mkuu.

"Hayo ni baadhi ya mambo makubwa yaliyofanywa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, Dk. John Pombe Magufuli na kukifanya chama kuwa na heshima na kuwa mfano wa kuigwa kwa vyama vingine vya siasa," alisema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba, Yussuf Ali Juma, alisema wanachama wa chama hicho mkoa wa kusini wamesikitishwa na kifo cha Mwenyekiti wao, Dk. Magufuli ambaye alifanya kazi kubwa kujenga chama na misingi yake hatua ambayo imekifanya chama hicho kukubalika Pemba.

Alisema ushindi mkubwa uliopata Chama Cha Mapinduzi katika majimbo ya Pemba kwa mara ya kwanza katika historia ya uchaguzi mfumo wa vyama vingi kwa nafasi ya uwakilishi na ubunge ni kielelezo cha kukubalika chama hicho Pemba.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## MAGODOWN YANAUZWA / YANAKODISHWA :

Kwa mahitaji ya kununua / kukodisha Magodown. Wasiliana na Tanlands Real Estate Agency (TREA) SIMU: 0628 336736 / 0688 373022

## YADI ZINAUZWA KURASINI / KIGAMBONI / CHAMAZI / CHANIKA

Ukubwa wa Yadi kuanzia SQM 4000, SQM 6000 mpaka SQM 8000. TANLANDS SIMU NO: 0628 336736 / 0686 302219

## MAENEO YA KUJENGA VITUO VYA MAFUTA (PETROL STATIONS PLOTS) YANAUZWA

Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma na Singida. TANLANDS SIMU: 0628 336736 / 0754 502757

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa*
*Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **ALHAJI S MSTAPHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari namba **T 270 CUE.** Taarifa za kupotea kwa kadi hiyo zimefunguliwa kituo cha Polisi Bukoba na kupewa jarada lenye namba **KAG/BUK/RB/146678/2021.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJ

**BENARD SIMBEYA SIMBEYA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA **BAJAJ AINA TVS KING** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC.720 AMX** CHASSIS NAMBA **MD2A5BZ2DWL96453.YE**YOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/157923/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA J/PCF.50**

**HATI YA KUUZA MALI KWA KUTIMIZA HUKUMU**

**(HCR/63)**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**

**MADAI No.140/2020.**

**Mdai.............................. SOSTHENES MATHIAS**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa........................... NUNGA JOSEPH MWITA**

**Kwa: ROYAL RUNNERS GENERAL SUPPLIES S.L.P 1045 DODOMA.**

Hati hii ya KUAMURU kuuza katika Mnada wa Hadhara, baada ya kutoa notice kwa muda wa siku 14 na muda wake kuishakuisha, **TUNATANGAZA KUUZA NYUMBA ILIYOPO NDACHI DODOMA MJINI PLOT NO 742 BLOCK 'A' MALI YA NUGA JOSEPH MWITA ILI KUFIDIA DENI ANALODAIWA NA SOSTHENES MATHIAS. MNADA HUO UTAFANYIKA TAREHE 20/04/2021 SAA 10:00 ASUBUHI.**

**KWA MAWASILIANAO;**
**0713913150 Au 0688729841.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**HATI YA KUUZA MALI KWA KUTIMIZA HUKUMU**
**(HCR/62)**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE DODOMA MJINI**

**MADAI No.67/2019.**

**Mdai.................. MWAJABU MOHAMED**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa......................... RUBA SHABANI**

**Kwa: ROYAL RUNNERS GENERAL SUPPLIES S.L.P 1045 DODOMA.**

Hati hii ya KUAMURU kuuza katika Mnada wa Hadhara, baada ya kutoa notice kwa muda wa siku 14 na muda wake kuishakuisha, **TUNATANGAZA KUUZA NYUMBA HIYO ILIYOAMRIWA NA MAHAKAMA ILIYOPO CHANG'OMBE EXTASITION PLOT NN 58 ILI KAGAWA KWA WADAWA YAANI MDAI NA MDAIWA 50% KWA 50%. MNADA HUO UTAFANYIKA TAREHE 27/03/2021 SAA 10:00 ASUBUHI.**

**KWA MAWASILIANAO;**
**0713913150 Au 0688729841.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.47/2021**

Ombi la STANSLAUS MTEMA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu
JUMA KISANJALA MTEMA
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 29/03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 23/3/2021



**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 83 YA MWAKA 2020**
**MAOMBI YA BARUZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**TUMSIFU ELIA SAWE-MAREHEMU**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**AGNESS TUMSIFU SAWE NA JUBLATE TUMSIFU SAWE**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**KANUNI YA 75**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 13 mwezi wa April 2021
Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 15 mwezi wa march mwaka 2021.



**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SUMMONS FOR DISPOSAL OF SUIT**
**(Rule 6. Subordinate Court (Civil Procedure-Summonses and Pleadings Rules, 1955)**
**In the District Court of Rungwe District**
**at Tukuyu**
**CIVIL CASE NO 7 OF 2020**
**Rungwe District Council .........Plaintiff**
**Versus**
**Ernest M. Mazigo and 7 others .... Defendant**
**To Alfred Albert**

.................................................................................
WHEREAS the above named plaintiff(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in the copy plaint with annexure attached hereto:
YOU ARE HEREBY SUMMONED to appear in this court in person or by an advocate duly instructed and able to answer all material question relating to suit or who shall be accompanied by some person able to answer such questions, on the 24 day of 03............2021 at 08:30 in the .................................. noon, to answer the claim, and as the day all the witness upon whose evidence and all the documents upon which you intend to rely in support of your defense.
Take notice; that if you do not appear on the day before the mentioned, the court shall, upon proof of service of the summons by affidavit of oral evidence pronounce judgement against you.
Given under my hand and the real of the court this 19 day of 03......2021



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA 114 YA 2014**
**BAINA YA**
**MUSTAFA JUMA TARANDU.................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**1. SHABANI ABDI**
**2. ABUSHEE ISSA JANKA**
**3. LEODGARD LEONARD SWAI.................WADAIWA**
**4. MCHINGA AUCTION MATR AND REAL CO.LTD**
**KWA: SHABANI ABDI**
**ABUSHEE ISSA JANKA**
**LEODGARD LEONARD SWAI**
**MCHINGA AUCTION MATR AND REAL CO.LTD**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza hili Wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 3.05.2021 saa 3:00 asubuhi. kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
ANGALIZO:- kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 23 ya mwezi Machi 2021.





Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yaweka vikwazo kwa maofisa Myanmar

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI jana imetangaza vikwazo dhidi ya maofisa wengine wawili wa Myanmar na kampuni mbili zenye uhusiano na jeshi la Myanmar.

Katika taarifa ya Wizara ya Fedha, Marekani ilisema vikwazo hivyo ni matokeo ya kampeni ya serikali inayoendelea na manyanyaso, vitisho dhidi ya waandamanaji wa amani na mashirika ya kiraia.

Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa na serikali ya Myanmar.

Jeshi lilichukua madaraka tarehe Februari, Mosi, mwaka huu katika mapinduzi na kuiondoa serikali ya kiraia na kumzuia kiongozi wa nchi Aung San Suu Kyi na maofisa wengine wa ngazi ya juu.

Mmoja ya waliowekewa vikwazo ni Than Hlaing, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Fedha, aliteuliwa kama mkuu wa Jeshi la Polisi na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani tarehe 2, Februari.

Mwingine ni Luteni Jenerali Aung Soe, ambaye wizara ya fedha ilisema ni kamanda wa idara ya operesheni maalumu na anaripoti moja kwa moja kwa kiongozi wa kijeshi wa Myanmar, Jenerali Min Aung Hlaing.

Waliochukuliwa vikwazo, mali wanazomiliki kwa asilimia 50 au zaidi ambazo ziko Marekani na kuwa mikononi au kudhibitiwa na raia wa Marekani zitazuiliwa.

EU pia ilitoa taarifa ya kuzuia mali za kiongozi wa kijeshi, Min Aung Hlaing na marufuku ya kutopewa Visa yeye na maofisa wa ngazi ya juu katika jeshi pamoja na kiongozi wa tume ya taifa ya uchaguzi.

VOA



Mtoto Anthony McClain Jr, akifuta machozi katika mkutano wa waandishi wa habari jana, kuzungumzia hatima ya kesi kuhusu mauaji ya baba yake Anthony McClain nje ya Idara ya Polisi ya Pasadena, California, Marekani. McClain aliuawa mwaka jana na polisi, familia yake inadai uwajibikaji wa wahusika wa tukio hilo. PICHA: REUTERS

# Guterres asisitiza ulinzi wa maji

**New York,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amesema hali ya hewa na maji havitengamani na kimoja hakiwezi kuwepo bila kingine, vivyo hivyo katika maisha ya binadamu.

Guterres aliyasema hayo katika ujumbe wake wa siku katika kuadhimisha siku ya utabiri wa hali ya hewa duniani jana.

Alisema mvuke kutoka kwenye uso wa dunia kwenda angani, husafirishwa kote ulimwenguni na kisha kuleta mvua na theluji ambayo hurudisha majisafi kwenye ardhi ya dunia, mito, maziwa na barafu.

Guterrres aliongeza hali hiyo ndio inayoendesha maisha kwenye dunia, kwa kuwa hali ya hewa husukuma mzunguko wa maji na kutabiri hali ya hewa ya dunia.

Katika ujumbe huo Guterres pia alisisitiza kuwa mzunguko huu mara nyingi huchukuliwa kuwa ni wa kawaida.

"Lakini ni kitovu cha malengo yetu mengi ya maendeleo endelevu kuanzia katika kutokomeza njaa, kuhakikisha afya na ustawi, kuwezesha viwanda vyenye tija, kudumisha jamii zinazostawi na kufungua uwezo wa kuwa na nishati nafuu na safi kwa wote," alisema Guterres.

Hata hivyo alionya kwamba mabadiliko ya tabianchi yanavuruga mzunguko huo na kugawanya uwezo wa upatikanaji wa maji kote duniani.

"Hii inamaanisha ongezeko la mafuriko kwa wengine na ukame wa muda mrefu kwa wengine, dunia yetu tayari inakabiliwa na changamoto lukuki za maji kuanzia matumizi yasiyo endelevu.

Nusu ya watu wote duniani wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa takribani mwezi mmoja kwa mwaka.

"Wakati mahitaji ya kimataifa ya maji yakiendelea kuongezeka tunakabiliwa za dhahma kubwa ya maji," alisema Katibu Mkuu UN.

"Tunahitaji kudhibiti hali ya hewa na maji katika njia iliyoratibiwa na endelevu ili kushughulikia usambazaji wa maji na changamoto za maji mengi kupita kiasi, machache kupita kiasi au yaliyochafuliwa kupindukia."

Guterres aliitaka dunia kuthamini uhusiano uliopo baina ya hali ya hewa na maji na umuhimu wa mzunguko wa maji.

Alisema pia kuongezwe juhudi za kuzisaidia jamii na hali ya hewa ili kuendeleza usimamizi mzuri wa vyanzo vya maji.

Alihitimisha ujumbe wake akisema "Hebu na tuhesabu kila tone la maji, kwa sababu kila tone lina umuhimu.

UN

## UN yaungana na EAC kumwomboleza Magufuli

**New York** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa (UN), umeungana na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambazo zinaendelea kupeperusha bendera za nchi zao nusu mlingoti, kwa siku 14 kwa ajili ya kuombeleza na Watanzania kufuatia kifo cha Hayati Dk. John Magufuli.

UN ilisema jana kuwa bendera itapepea nusu mlingoti kwenye makao makuu yake kuanzia keshokutwa, kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania Hayati John Pombe Magufuli, kufuatia kifo chake Machi 17, mwaka huu.

Ofisi ya Itifaki ya UN, ilisema ofisi zote za UN duniani zimehimizwa kufanya hivyo pia, taarifa iliyotolewa jana kwenye ukurasa wa twitter wa UN, ilisema.

Hayati Magufuli anakuwa ni rais wa kwanza Tanzania, kufariki akiwa madarakani ikiwa ni awamu ya tano ya uongozi wa urais nchini humo.

Magufuli alifariki dunia kwa tatizo la moyo, kifo kilichotangazwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Hayati Magufuli atazikwa keshokutwa, kijijini kwake Chato katika Mkoa wa Geita, uliopo Kanda ya Ziwa, nchini Tanzania.

BBC

## Shambulio kijiji Niger laua 137 Niamey, NIGER

**Niamey,** NIGER

SERIKALI nchini Niger imesema kuwa idadi ya watu waliotambuliwa kuuawa katika shambulio la mwishoni mwa wiki, imefikia 137.Shambulio hilo linashukiwa kutekelezwa na wanamgambo wa Islamic State (IS).Vijiji vitatu vililengwa katika shambulio hilo, karibu na mpaka na nchi jirani ya Mali.Niger inakabiliwa na misururu ya mashambulio ya kushtukiza yanayofanywa na wanamgambo wa Kiislamu ambao hufanya uvamizi wa kushambulia na kutoweka dhidi ya vijiji vilivyo mbali kwa kutumia pikipiki na magari aina ya pick-up.Ilibainika shambulio hilo dhidi ya vijiji vilivyopo kwenye mpaka wa Nijer, Mali na Burkina Faso lilikuwa baya na zaidi ya 130 waliuawa.Kumekuwa na mashambulio ya aina hii katika eneo jingine la mapambano ambapo wanajeshi wa Mali waliuawa wiki moja kabla.Niger ni sehemu iliyo chini ya muungano wa nchi zinazoiunga mkono Ufaransa katika ukanda wa Sahel unaofahamika kama G5.Kikosi cha wanajeshi 1,200 kutoka jeshi la Chad, kinachotazamwa kama kikosi chenye nguvu zaidi, kimepelekwa kusaidia kukabiliana na tishio la mashambulizi hayo ya wanamgambo.

BBC

# BIFU LA IBRAHIMOVIC, LEBRON LAENDELEA

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, ameendelea kukoleza moto kuhusu ugomvi wake wa kurushiana maneno na nyota wa kikapu nchini Marekani, LeBron James.

Ibrahimovic ameendelea kumpasha LeBron kwamba, wanamichezo hawapaswi kujiweka mbele katika masuala ya siasa.

Nyota huyo wa Sweden amekuwa akimkosoa vikali LeBron ambaye kwa sasa amejipa jukumu la kuwa balozi wa watu weusi nchini Marekani katika kupingana na vitendo vya ubaguzi wa rangi wanavyofanyiwa Wamarekani weusi.

"Wanamichezo wanaunganisha dunia, siasa zinaigawanya, jukumu letu ni kuunganisha ulimwengu kwa kufanya mambo ambayo yataunganisha jamii," aliandika Ibrahimovic kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Wanamichezo wanapaswa kuwa wanamichezo na wanasiasa wanapaswa kuwa wanasiasa," aliongeza Ibrahimovic.

Hata hivyo, LeBron ameendelea kumkosoa Ibrahimovic na kusisitiza kuwa hawezi kunyamaza juu ya mambo mabaya wanayofanyiwa watu weusi, kwani yeye pia ni mhanga.

"Sitaweza kunyamaza kwa hili, Ibrahimovic ndio anapaswa kufunga mdomo wake," alijibu LeBron kupitia Twitter yake.




## DESCHAMPS AIONA NAFASI DEMBELE KUWIKA UFARANSA

**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps anaamini Ousmane Dembele, bado anaweza kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi cha Ufaransa, baada ya kumuita tena mshambuliaji huyo kwa ajili ya michuano ya kufuzu Kombe la Dunia.

Dembele hajacheza mechi za kimataifa tangu Novemba 2018, wakati alipoingia akitokea benchi kwenye mchezo wa Kombe la Ligi ya Mataifa ya Uefa waliochapwa mabao 2-0 na Uholanzi.

Hata hivyo, kiwango chake msimu huu kule Barcelona kimemfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kuitwa tena kwenye kikosi hicho cha 'Les Bleus' kwa mchezo wa Kundi D dhidi ya Ukraine, Kazakhstan na Bosnia-Herzegovina.

Deschamps alimpa nafasi ya kuanza kuichezea Ufaransa Septemba mwaka 2016, na sasa anaamini kwamba, Dembele anaweza kuwa na mchango mkubwa kwa kikosi hicho.

"Yeye ni mchezaji ambaye ameonyesha ubora wake mapema sana. Bado kijana," alisema Deschamps akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu.

"Kama unataka kumuona yeye ni wakati ambao hajaandamwa na majeruhi, kwani anakuwa bora sana.

"Sasa yupo tayari kucheza tena, yupo tayari kutengeneza tofauti na kufunga mabao. Anaweza kufunga zaidi na kuwa na mchango mkubwa zaidi kwa kikosi chetu.

Dembele amefunga mabao tisa na kutoa pasi za mwisho nne kwa Barca kwenye mashindano yote msimu huu akiwa kwenye msimu wake wa nne pale Camp Nou.

## TOTTENHAM YAMWINDA KIPA WA MAN UNITED

**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur inawania kumsajili golikipa wa Manchester United, Dean Henderson, ili kurithi mikoba ya mlinda mlango wao wa sasa, Hugo Lloris, kwa mujibu wa Sky Sport.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka ndani ya timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England, Spurs wanapiga hesabu za kumpata kipa mpya kwa sababu Lloris ana mpango wa kuondoka nchini Uingereza na anahitaji kwenda kucheza nyumbani kwao nchini Ufaransa.

Mkataba wake ndani ya kikosi hicho kinachonolewa na Kocha Jose Mourinho unamalizika mwishoni mwa msimu huu jambo ambalo linaongeza nguvu kwa Tottenham kusaka mbadala wake.

Henderson mwenye miaka 24, anatengenezwa ndani ya United kuwa mrithi wa David de Gea, ambaye amepewa chaguo la kufanya maamuzi anayotaka ndani ya timu hiyo kwa kile ambacho kimeelezwa kuwa ni kumpa heshima ya utumishi wake, kwani naye anahitaji kuondoka pia.

Na sasa Spurs wanaona kwamba Henderson ndio chaguo sahihi kwao na hivyo wapo kwenye mpango wa kutoa ofa kwa Man United wakati dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto litakapofunguliwa.

Lloris alijiunga na timu ya Tottenham msimu wa 2012 na amecheza jumla ya mechi 363.

## HABARI MICHEZO




# ZIDANE: HATUWACHUKULII POA LIVERPOOL UEFA

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema kuwa mchezo wao ujao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool utakuwa mgumu licha ya timu hiyo kutokuwa na mwenendo mzuri kwenye Ligi Kuu England.

'Los Blancos' hao wamepangwa dhidi ya kikosi cha kocha Jurgen Klopp katika hatua hiyo, ikikumbushia fainali ya mashindano hayo iliyopigwa katika msimu wa 2017-18 na Madrid kuibuka bingwa.

Liverpool kwa sasa hali yao ni mbaya ikishinda michezo minne tu tangu mwaka huu uanze, lakini Zidane amesema kuwa hatouchukulia mchezo huo kuwa ni mwepesi kwake.

"Tuna wakati mgumu, mchezo huu hautakuwa rahisi hata kidogo, na hakuna mechi rahisi, hivyo tutachukua tahadhari zote," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari.

"Hatuangalii sana matokeo kwenye Ligi Kuu England, maana mashindano haya ni tofauti na kila timu inaingia kwenye kila mchezo kwa ari tofauti.

"Wao (Liverpool) wanaweza kuwa na wakati mgumu kule England, lakini wakatoa upinzani mkubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, tunauchukulia mchezo huu kwa umakini wa hali ya juu zaidi."

# TUCHEL AMTULIZA ABRAHAM CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ameweka wazi kuwa alifanya mazungumzo na mshambuliaji wa timu hiyo, Tammy Abraham, akimshawishi aendelee kupambana.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 23,ameripotiwa kwamba, anataka kuondoka kwenye viunga hivyo vya Stamford Bridge wakati wa majira ya joto mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo amekuwa akipambana kujihakikishia namba kikosi cha kwanza hasa kutokana na ushindani mkubwa, lakini kutokana na jeraha kwenye kifundo cha mguu, inamlazimu kukaa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Olivier Giroud.

"Tulikuwa na mazungumzo naye mara kadhaa ya kumtia moyo asikate tamaa," alisema Tuchel akinukuliwa na BBC Sport.

"Tumemwambia akubaliane na hali halisi, asiwaze sana, bali arejee katika hali ambayo haitampa mawazo," aliongeza Tuchel.

Mshambuliaji huyo kwa sasa amepona jeraha hilo na alikuwapo kwenye mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Sheffield United Jumapili iliyopita ambapo Chelsea walifuzu kutinga nusu fainali.

# INGS

## KUMRITHI AGUERO CITY

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City inafikiria uhamisho wa straika nyota wa Southampton, Danny Ings, kwa mujibu wa Sky Sports.

Huku Sergio Aguero akionekana kuwa ataondoka mwishoni mwa msimu huu, Pep Guardiola anataka kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Na sasa Ings anaonekana kuwa ndiye chaguo sahihi na atapatikana kwa bei ndogo, tofauti na straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland.

Aguero ambaye ni mfungaji wa wakati wote wa Man City, mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na hakuna dalili yoyote inayoonyesha kwamba, anaweza kuongezewa mkataba mwingine hapo kwenye dimba la Etihad.

Guardiola licha ya kuvutiwa zaidi na Haaland, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, Barcelona, Manchester United, Chelsea, Paris Saint-Germain, Liverpool na Juventus, lakini bei yake ndio kikwazo.

Kwa mujibu wa ripoti, Guardiola anaona kuwa Ings ambaye, ni mshambuliaji wa zamani wa Liverpool atakuwa rahisi kumpata na kwa bei nafuu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND AVUNJA UKIMYA KUONDOKA DORTMUND

Bado nina mkataba wa miaka mitatu hapa, sina wasiwasi juu ya hilo kwani...

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland amevunja ukimya kuhusu uvumi wa majaliwa yake, akisisitiza ana miaka mitatu imebaki kwenye mkataba wake na Borussia Dortmund.

Haaland ameendelea kuhusishwa na klabu kubwa za Ulaya zikiwamo timu kama Real Madrid, Manchester City, Barcelona, Manchester United, Chelsea, Juventus, Paris Saint-Germain na Liverpool.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye aliulizwa kuhusu majaliwa yake wakati akiwa kwenye majukumu ya timu ya Taifa ya Norway, wakijiandaa kucheza na Gibraltar leo kwenye mchezo wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia.

Ofa nyingi za fedha zinasemekana ziko mbioni, lakini Haaland amesema ataendelea kuziba masikio kwa uvumi huo na kuweka umakini kwenye kikosi chake kwa sasa.

Akihojiwa juu ya uvumi huo kwenye mkutano na waandishi wa habari, Haaland alisema: “Bado nina mkataba wa miaka mitatu pale Dortmund. Sina wasiwasi juu ya hilo.”

Haaland, ambaye alijiunga na Dortmund akitokea kwa mabingwa wa Austria, Salzburg, Januari mwaka jana, alifunga mara mbili kwenye mchezo wa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Cologne, Jumamosi.

Amefikisha mabao 14 ugenini kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga msimu huu, zaidi ya iliyofunga Werder Bremen (13), Hertha Berlin (13), Mainz (11), Arminia Bielefeld (10) na Schalke (nane).

Haaland amefunga mabao 21 kwenye mechi 21 za Ligi kuu msimu huu na 33 kwenye mashindano yote.

## KWA UFUPI

**INGS KUTUA MAN CITY**
MSHAMBULIAJI wa Southampton, Danny Ings, mwenye umri wa miaka 28, anawaniwa na Manchester City kuichukua nafasi ya Sergio Aguero. ***(Sky Sports)***

**DE BEEK SASA KUUZWA**
MANCHESTER United inaweza kumuuza kiungo wake wa kati mwenye umri wa miaka 23, Donny Van de Beek, ili kupata fedha za kufanikisha usajili msimu wa majira ya joto. ***(90 min)***

**DAKA AWINDWA EPL**
MSHAMBULIAJI wa Zambia, Patson Daka, mwenye umri wa miaka 22, ambaye amefunga mabao 20 katika mechi 18 kwenye klabu ya Austria, Red Bull Salzburg, msimu huu, anazivutia klabu za Manchester United, Manchester City, Liverpool na Arsenal. ***(Mail)***

**OCAMPOS KUTUA WOLVES**
WOLVES wana nia ya kumsajili winga wa Sevilla raia wa Argentina, Lucas Ocampos mwenye umri wa miaka 26, kwa kiasi cha pauni milioni 62 zilizopo katika kifungu cha mkataba wake. ***(Football Insider)***

**INTER YAMTAKA ORIGI**
INTER Milan wanafikiria kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Mbelgiji Divock Origi mwenye umri wa miaka 25, ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(Calcio Mercato - in Italian)***

**AOUAR KUTUA JUVENTUS**
KIUNGO wa kati wa Lyon, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, atajiunga na Juventus kipindi cha majira ya joto. ***(FourFourTwo via Tuttospor)***

**MILAN NAYO KWA VLAHOVIC**
AC Milan imeripotiwa kujiunga na Tottenham katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Fiorentina, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, katika kipindi cha majira ya joto. ***(La Reppublica via Teamtalk)***

**VARANE AMVUTA MBAPPE REAL**
MLINZI wa Ufaransa, Raphael Varane, amesema angependa kuungana na mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, pale Real Madrid, mchezaji ambaye anamwona kuwa “bora zaidi katika soka” barani Ulaya. ***(Europe1 via Goal)***

**VILLA KUMUUZA WESLEY**
ASTON Villa wako tayari kupokea ofa wakati wa kipindi cha uhamisho cha majira ya joto kwa mshambuliaji wao, Wesley Moraes mwenye umri wa miaka 24 . ***(Football Insider)***

**ARMSTRONG AWANIWA NEWCASTLE**
ADAM Armstrong mwenye umri wa miaka 24, anawindwa na klabu yake ya zamani, Newcastle ambayo ingependa kumrudisha mshambuliaji huyo pale St James Park kutoka Blackburn Rovers. ***(Teamtalk)***

**AANHOLT HUYO GALATASARAY**
KLABU ya Galatasaray ya Uturuki imempa nafasi ya kujiunga nao msimu ujao mlinzi wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 30, Patrick van Aanholt. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

# MWAMBUSI AIREJESHA YANGA KAMBINI KUJIWINDA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amesema kikosi cha timu hiyo leo kitaingia kambini tayari kwa maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Kombe la FA.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 50 baada ya mechi 23, inatarajia kuikaribisha KMC FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Machi 7, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema wanarejea kuendelea na programu za maandalizi, wakitokea kwenye mapumziko mafupi kupisha kuagwa kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Alisema leo, wataendelea na programu ya mazoezi kwa wachezaji wake ambao ameanza kufanya nao mazoezi wiki iliyopita na kuhakikisha anafanyia kazi upungufu aliouona ndani ya kikosi hicho.

"Tutaendelea na mazoezi ya kawaida kwa sababu timu iko vipande vipande, sasa nitaendelea na zoezi la kutengeneza muunganiko wa jumla na kuwapa programu maalum washambuliaji.

"Hakuna upungufu mkubwa sana, kikubwa ni umakini tu hasa kwa nafasi ambazo wanatengeneza kuzigeuza kuwa mabao ili kupata ushindi, lakini pia kuwasisitizia mabeki kuongeza umakini katika kulinda lango," alisema Mwambusi.

Alisema mikakati yake ni kuendelea kuimarisha kikosi cha timu hiyo na kuwa tayari kwa Ligi Kuu Tanzania iliyosimama kupisha kalenda ya Fifa kwa timu ya taifa kucheza mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021.

Kocha huyo alisema ana imani watakuwa sawa timu itakapokamilika kwa baadhi ya nyota wake waliopo timu za taifa watakapomaliza majukumu yao ya kitaifa na kurejea.

## Morocco aiandalia mauaji Nkana FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuanza vibaya mechi mbili za awali za hatua ya makundi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema anaufanyia kazi ubora na udhaifu wa wapinzani wao Nkana FC, ambao wanatarajia kucheza nao Aprili 4, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema amefanikiwa kuona ubora na udhaifu wa Nkana, hivyo anaendelea kuufanyia kazi kwa kuhakikisha wanapata matokeo chanya kwenye mchezo huo.

Alisema Nkana ni timu nzuri pia na inazoefu wa mashindano hayo, hivyo wana kazi kubwa kuhakikisha wanajiandaa na kufanyia kazi udhaifu wa wapinzani wao ili kupata matokeo.

"Nkana ni timu nzuri, japo hawajapata matokeo kama sisi tunajuwa watakuja hapa kutaka matokeo, lakini na sisi tunahitaji kupata matokeo, tuko sawa kwa mechi hiyo.

"Tunaendelea kufanyia kazi udhaifu wetu ikiwamo suala la ushambuliaji kumalizia nafasi tunazotengeneza, lakini pia katika safu ya ulinzi, mabeki kutokuwa makini na kama ilivyo kwa mechi iliyopita dhidi ya Pyramids FC," alisema Morocco.

Namungo FC ambayo ipo Kundi D, katika michuano hiyo, imepoteza mechi zake mbili za mwanzo dhidi ya Raja Casablanca ugenini ilipokubali kipigo cha bao 1-0 nchini Morocco na kisha kuangukia pua ya mabao 3-0 nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Pyramids ya Misri.

Matokeo hayo yanaiweka Namungo katika nafasi ngumu ya kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoshika nafasi ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa.

**HUZUNI...**



Mwimbaji maarufu wa muziki wa Taarab, Khadija Kopa, akiimba kwa huzuni kubwa wimbo wa maombolezo wakati wa kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# AS Vita yampasua kichwa Gomes, Simba

**Na Saada Akida**

HUKU akiendelea kuwanoa wachezaji ambao hawajaitwa kuzitumikia timu zao za taifa kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema anatambua mchezo dhidi ya AS Vita hautakuwa rahisi na kukitaka kikosi chake kutuliza akili na nguvu zao kuelekeza kwenye mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba inaongoza Kundi A ikiwa na pointi 10 ikifuatiwa na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri yenye pointi saba huku AS Vita ya DR Congo ikiwa na alama nne na Al-Merrikh ya Sudan ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

Mechi ijayo, Simba itaikaribisha AS Vita Aprili 3, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam baada ya mechi ya awali zilipokutana DR Congo, Wekundu wa Msimbazi hao kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Baada ya mchezo huo, Simba ambayo inahitaji pointi moja tu ili kufuzu hatua ya robo fainali, itasafiri kwenda nchini Misri kuivaa Al Ahly Aprili 9, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema mechi zilizobakia mbele yao ni ngumu na wanahitaji kuwa makini hasa mechi nyumbani kuhakikisha wanapata pointi ambayo itawapa nafasi ya kucheza robo fainali.

Alisema ameongea na wachezaji kwamba haitakuwa kazi nyepesi kwao kwa sababu kila timu inahitaji ushindi, na muhimu kwao ni kupambana kutafuta matokeo katika mchezo wa nyumbani dhidi ya AS Vita.

"AS Vita ni wazuri, tumecheza nao kwao na kupata ushindi wa bao 1-0, pia nimewaona walivyocheza dhidi ya Al Ahly hautakuwa mchezo mwepesi, tunatakiwa kushinda.

"Ikiwa tutashindwa kupata matokeo katika mechi hiyo, itakuwa ngumu kwetu kufikia malengo ya hatua ya robo fainali na nimeongea na wachezaji tuwe tayari kupambana kufanya vizuri katika mchezo huo," alisema Gomes.

Alisema wanaendelea na mazoezi kwa wachezaji ambao hawako katika majukumu ya timu ya taifa, kwa kuwa hakuna muda wa kupoteza kwani kilichobaki ni kupambana tu kutafuta ushindi katika mechi hiyo.

Jumla ya wachezaji 19 wa Simba wapo katika majukumu na timu zao za taifa ambao ni Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohamed Hussein, 'Tshabalala' Kennedy Juma, Erasto Nyoni, Jonas Mkude, Hassan Dilunga, Mzamiru Yassin, Said Ndemla na John Bocco waliopo na kikosi cha Taifa Stars.

Wachezaji wa kigeni wanaozitumikia timu zao za taifa kutoka Simba ni Luis Miqussione (Msumbiji), Meddie Kagere (Rwanda), Rally Bwalya na Clatous Chama (Zambia), Joash Onyango na Francis Kahata (Kenya), Peter Muduhwa na Perfect Chikwende (Zimbabwe) na Taddeo Lwanga (Uganda).



HAALAND AVUNJA UKIMYA KUONDOKA DORTMUND HABARI UK 22

TUTAKOMAA...



Wachezaji wa timu ya soka ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, kiungo Mzamiru Yassin (kushoto) na mshambuliaji John Bocco, wakifanya mazoezi ya mwisho katika Uwanja wa Chuo cha Utalii, Nairobi nchini Kenya jana, kabla ya kusafiri kwenda Malabo, Equatorial Guinea kuvaana na wenyeji hao kwenye mechi ya Kundi J kuwania kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon. **MPIGAPICHA WETU**

## KAGERE, MIQUISSONE WAVAANA AFCON

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Simba, straika Meddie Kagere na kiungo mwenzake wa klabu hiyo leo watakuwa wakipambana kila mmoja akitaka kuipa heshima timu yake ya taifa kwenye kinyang'anyiro cha kusaka nafasi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajia kufanyika Cameroon.

Kagere akiwa na timu yake ya Taifa ya Rwanda, leo atakuwa nyumbani nchini humo, akimkaribisha Miquissone na kikosi cha timu ya Msumbuji ambacho kimesafiri hadi huko kusaka pointi tatu kwa ajili ya kujiwekea mazingira mazuri ya kufuzu.

Mechi hiyo ambayo itachezwa kwenye Uwanja wa Nyamirambo majira ya saa 10:00 kwa saa za Afrika Mashariki, Rwanda itakuwa ikitaka kulipa kisasi baada ya mchezo wa awali zilipokutana Novemba 14, mwaka jana, Msumbiji kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

Itakuwa ni mechi ya Kundi F, linaloongozwa na Cameroon, ambayo ina pointi 10 kwa mechi nne ilizocheza, Msumbuji ikishika nafasi ya pili kwa pointi nne, ikicheza mechi nne, Cape Verde ikiwa nafasi ya tatu kwa pointi nne pia huku Rwanda wao wakiburuza mkia wakiwa na pointi mbili tu kwa mechi nne ambazo wamecheza.

# NTIBAZONKIZA FITI KUIBEBA YANGA

●●●Kumalizana kwanza na Wamorocco kuwania kufuzu Afcon kabla ya kuiwahi KMC FC huku...

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga na timu ya Taifa ya Burundi, Saidi Ntibazonkiza, kwa sasa yupo fiti kurejea kuitumikia Yanga kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Bara pamoja na Kombe la FA, imefahamika.

Ntibazonkiza ambaye kwa mara ya mwisho kuichezea Yanga ilikuwa Januari 13, mwaka huu, kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar, amekuwa nje tangu kipindi hicho akiuguza majeraha ya nyonga.

Lakini kwa sasa yupo fiti na Kocha wa timu ya Taifa ya Burundi, Jimmy Ndayizeye, amemjumuisha katika kikosi chake kinachotarajiwa kuivaa Jamhuri ya Afrika ya Kati keshokutwa, Ijumaa kwenye mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon).

Hata hivyo, kauli ya daktari wa timu hiyo ya taifa ilizua gumzo, baada ya kueleza kuwa nyota huyo hakuwa na majeraha kama ilivyoripotiwa na klabu yake kipindi alipoitwa na kocha wa timu ya Taifa ya Burundi, Ndayizeye.

Ntibazonkiza ambaye hadi sasa ameifungia Yanga mabao mawili kwenye Ligi Kuu Bara na kutoa pasi tatu za mwisho, kwa kipindi chote ambacho amekuwa nje ya uwanja akijiuguza, safu ya ushambuliaji ya timu yake imekosa makali, hivyo kurejea kwake huenda ikawa faraja husussan ni wakati wakiivaa KMC FC Aprili 7, mwaka huu.

Yanga ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 50 baada ya michezo 23, huduma ya Ntibazonkiza ni muhimu katika kipindi hiki ambacho klabu hiyo inahitaji kuendelea kushinda ili kutimiza malengo yake ya kutwaa ubingwa msimu huu.

Miamba hiyo itaingia kambini leo baada ya mapumziko mafupi ya kutoa nafasi kwa wachezaji wake kuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ambaye anatarajiwa kuzikwa nyumbani kwao, Chato mkoani Geita keshokutwa, Ijumaa.

Hata hivyo, Ntibazonkiza kujiunga na klabu yake, itakuwa ni baada ya mwishoni mwa mwezi huu kutokana na Burundi kukabiliwa na mechi mbili za kuwania kufuzu Afcon, ambapo Ijumaa itaikaribisha Jamhuri ya Afrika ya Kati kabla ya Machi 30, mwaka huu kuifuata Morocco.

Burundi ipo Kundi E ikiwa nafasi ya tatu na pointi zake nne huku Morocco yenye alama 10 ikiwa kileleni ikifuatiwa na Mauritania yenye pointi tano na Jamhuri ya Afrika ya Kati ikiburuza mkia kwa alama tatu.

Mechi hiyo kati ya Burundi na Jamhuri ya Afrika ya Kati ilikuwa ipigwe nchini katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, lakini Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeurudisha mchezo huo jijini Bujumbura, Burundi.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Soka nchini Tanzania (TFF), mechi hiyo imerudishwa nchini Burundi, baada ya CAF, kuruhusu kutumika kwa Uwanja wa Intwari jijini Bujumbura.

Awali Shirikisho la Soka la Burundi (FFB), liliiomba TFF pamoja na serikali kuruhusu mechi yao ichezwe nchini Tanzania baada ya CAF kuufungia uwanja huo ambao ndiyo unakidhi vigezo vya kimataifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002

HABARI KITAIFA

ANNA MWAKASEGE:

# Aliyerusha ndege iliyobeba mwili wa JPM

**Na Romana Mallya**

WAKATI Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki ikishuhudia mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya urais, Shirika la Ndege (ATCL) linajivunia hazina ya marubani wake, wakiwamo wanawake.

Machi 19, mwaka huu, Tanzania iliweka rekodi pale Samia Suluhu Hassan alipoapishwa kuwa Rais wa kwanza mwanamke ukanda wa Afrika Mashariki.

Wakati mwili wa Rais Magufuli ukiondolewa Dar es Salaam Jumapili kupelekwa makao makuu ya nchi jijini Dodoma, ndege ya aina ya Air Bus 220-300 ya Shirika la ATCL iliyoubeba, ilikuwa chini ya uongozi wa rubani mwanamke, Anna Mwakasege.

Ni rubani wa muda mrefu ndani ya shirika hilo, lakini amepata umaarufu mkubwa katika mitandao ya kijamii baada ya tukio la kurusha ndege hiyo ikiwa na mwili wa Rais John Magufuli kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Anna amewahi kufanyiwa mahojiano na moja ya majarida yanayochapishwa na ATCL na ndani yake alibainisha alivyotimiza ndoto yake ya kuwa rubani.

Katika jarida hilo, Anna anasema alianza safari ya kutimiza ndoto yake hiyo akiwa na umri mdogo wa elimu ya msingi, akipenda dhana ya kurusha chombo kwenye mawingu.

"Ninapenda kazi yangu. Ninafurahia kila safari ninayoifanya," anasema na kubainisha kuwa abiria wengi hufurahia wanapomwona na anaamini wanathamini anachokifanya kwa kuwa marubaini wanawake si wengi duniani.

Katika jarida hilo, Anna aliulizwa kuhusu dhana iliyojengeka kwamba wanawake wanakuwa marubani wazuri zaidi, akijibu:

"Sina uhakika kama wanawake tuna faida kubwa katika hilo. Wanaume na wanawake wana tofauti, inategemea na mazingira."

Anna anasema kupitia kazi yake hiyo, amepata mafanikio makubwa na kama akitakiwa kutaja mojawapo, ni siku aliyofaulu mtihani wa kuwa rubani wa kurusha ndege aina ya Airbus.

"Kufaulu mitihani ilikuja baada ya muda mfupi kumpoteza mdogo wangu wa kiume na kilikuwa ni kipindi kigumu. Kufaulu mtihani ilinipunguzia hisia na machungu niliyokuwa nayo na kurudisha furaha yangu," alisema.

## Bendera UN nusu mlingoti

**Na Romana Mallya**

UMOJA wa Mataifa (UN) umetangaza kupeperusha bendera nusu mlingoti katika ofisi za makao makuu zilizopo jijini New York, Marekani wakati wa maziko ya Rais John Magufuli yanayotarajiwa kufanyika Ijumaa, Chato mkoani Geita.

Kwa mujibu wa taarifa ya UN iliyotolewa jana kwenye ukurasa wake rasmi wa mtandao wa kijamii wa Twitter, Ofisi ya Itifaki ya umoja huo imeagiza ofisi zote za UN duniani kufanya hivyo ili kumuenzi Rais Magufuli aliyefariki dunia Jumatano ya wiki iliyopita mkoani Dar es Salaam.

"Bendera ya Umoja wa Mataifa itapeperusha nusu mlingoti kwenye Makao Makuu ya UN Ijumaa Machi 26 kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli, kutokana na kifo chake," UN ilibainisha katika taarifa yake hiyo.

Rais Magufuli alifariki dunia Jumatano iliyopita saa 12 jioni katika Hospitali ya Mzena mkoani Dar es Salaam kutokana na maradhi ya moyo yaliyomsumbua kwa zaidi ya miaka 10.

## Waliofariki dunia Uwanja wa Uhuru kuzikwa pamoja

**Na Mary Geofrey**

WATU watano wa familia moja waliopoteza maisha katika shughuli ya kuuaga mwili wa Hayati Rais John Magufuli Jumapili katika Uwanja wa Uhuru mkoani Dar es Salaam, watazikwa kesho katika makaburi ya familia eneo la Kimara Mwisho.

Waliopoteza maisha ni mama na watoto wake wawili na watoto wengine wawili wa shemeji zake.

Akizungumza na Nipashe jana, mume wa marehemu, Denis Mtua, aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni mke wake, Suzan Ndana (34), watoto wake Natalia Mtua (7) na Nathan Mtua (8).

Alisema wengine ni watoto wa kaka zake wawili ambao ni Christian Allan Mtua (10) na Michelle Mtua (9).

"Miili yote tutaipumzisha sehemu moja katika eneo la familia nyumbani Kimara saa 9:00 alasiri, ibada ya kuwaaga itatangulia katika Kanisa la KKKT Usharika wa Kimara lililopo Korogwe, kuanzia 6:00 mchana," alisema Mtui.

Alisema pamoja na familia hiyo, mke wake aliongozana na dada wa kazi aliyefahamika kwa jina moja la Anitha ambaye mpaka jana alikuwa hajapatikana.

"Tumemtafuta katika hospitali na mochwari za hospitali bila ya mafanikio, tunaendelea na juhudi za kumtafuta," alisema Mtui.

Alisema wamefanikiwa kumpata ndugu wa dada huyo wa kazi na leo wanatarajia kwenda kumwangalia katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI), ambako majeruhi wengine walipelekwa.